MKUTANO WA TANO

Kikao cha Kwanza – Tarehe 12 Oktoba. 2011

(Kikao kilianza Saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA SPIKA

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tutakuwa na taafira mbili mbaka tatu za Spika, moja ni taafira inayohusu shughuli zetu za kazi ya kupitisha Miswada, nyengine ni taarifa inayohusu misiba iliyotokezea katika nchi yetu.

Waheshimiwa Wajumbe katika Mkutano wa Nane wa Baraza la Wawakilishi uliofanyika kuanzia tarehe 15 Juni, 2011 hadi tarehe 31 Julai, 2011. Baraza lilipitisha Miswada mitatu ya Sheria kama ifuatavyo:

1. Mswada wa kwanza

   Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Shilingi bilioni 613,076,406 kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa mwaka wa fedha unaoushia siku ya tarehe 30 Juni, 2012 na kuruhusu utoaji na uhaulishwaji wa fedha hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

2. Mswada wa pili

   Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar, kazi zake na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

3. Mswada wa Tatu

   Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Utawala, Udhibiti, Uendeshaji wa Viwanja vya Ndege Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Waheshimiwa Wajumbe kama inavyotakiwa chini ya kifungu cha 90 kifungu kidogo cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2011, naomba kutoa taarifa kwamba Miswada hiyo

imekuwa ni sheria kamili baada ya kusainiwa na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi.

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wajumbe.

TAARIFA KUHUSU MISIBA ILIYOTUFIKA KATIKA NCHI YETU

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe kwa huzuni kubwa majonzi na masikitiko naomba kuwaarifa kwamba mnamo siku ya Jumaane tarehe 23 Agosti, 2011 Baraza letu la Wawakilishi Zanzibar lilipata msiba wa kuondokewa na Mheshimiwa Mwenzetu aliyekuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Uzini Unguja. Mhe. Mussa Khamis Silima, ambae alipata ajali ya gari yeye na mkewe tarehe 21 Agost, 2011 nje kidogo ya Mji wa Dodoma na alifariki dunia tarehe 23 Agosti mwaka huu, kwenye hospitali ya Taifa Muhimbili Dar es Salaam.

Mke wake yeye alifariki pale pale kwenye ajali hiyo siku ya tarehe 21 Agosti, 2011. Marehemu Mhe. Mussa Khamis Silima alizikwa siku ya Jumatano tarehe 24 Agost,2011 kijijini kwao Kiboje Mwembeshauri Wilaya ya Kati Unguja.

Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa maelekezo ya kifungu cha 71 kifungu kidogo cha pili cha katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, toleo la mwaka 2010 nilichukua hatua tarehe 26 Mwezi wa Agosti mwaka huu ya kutoa taarifa rasmi ya kifo hicho kwa Mheshimiwa Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar, kwamba kiti cha Mjumbe Muwakilishi jimbo la Uzini kiko wazi kuanzia tarehe 23 Agost, 2011 ambapo Mhe. Mussa Khamis Silima alifariki.

Waheshimiwa Wajumbe kwa mujibu wa kifungu cha 71 kifungu kidogo cha pili cha katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na kwa mujibu wa kanuni namba 6 kanuni ndogo ya nne ya kanuni ya Baraza la Wawakilishi toleo la mwaka 2011. Naomba kuchukua nafasi hii kutangaza katika Baraza hili kifo cha Marehemu Mhe. Mussa Ame Silima sote kwa pamoja tumuombee Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi Amin.

Waheshimiwa Wajumbe vile vile kutokana na msiba mkubwa uliotokea wa kifo cha mwenzetu huyo Mhe. Mussa Ame Silima na ajali ambayo ilitokea tarehe 10 Septemba, 2011 ya kuzama kwa meli ya Spice Ilander kwenye mkono wa bahari ya Nungwi tulipokea salamu za pole na rambi rambi kutoka kwa watu na taasisi mbali mbali za kitaifa na kimataifa, naomba kuchukua nafasi hii kutoa shukurani zetu za dhati kwa wote waliotuletea salamu za pole na rambi rambi ambazo zilitufariji sana wakati wa kipindi hiki kigumu cha msiba na ishaalla Mwenyezi Mungu atawalipa kheri kwa ihisani na wema wao mkubwa wa kutupa pole na kutuunga mkono kwenye kiipindi hicho kigumu.

Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima kubwa naomba kuchukua nafasi hii kuzisoma mbele yenu kwenye Baraza hili baadhi ya salamu za pole na rambi rambi tulizoletewa kutokana na msimba huo mkubwa uliotufika.

Salamu kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Waheshimiwa Wajumbe salamu za kwanza kuhusiana na msiba wa Mhe. Mussa Khamis Silima zilitoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete ambazo zimesomeka kama ifuatavyo.

Mhe. Pandu Ameir Kificho Spika wa Baraza la Wawakilishi sanduku la posta 902 Zanzibar, nakuandikia kukufahamisha kuwa nimepokea kwa masikitiko na huzuni kubwa taarifa ya kifo cha Mhe. Mussa Khamis Silima aliyekuwa muwakilishi wa jimbo la uchaguzi la Uzini na Mbunge wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Baraza la Wawakilishi Zanzibar, kifo kilichotokea tarehe 23 Agost 2011 ni pigo kubwa kwa taifa kwa Bunga na Baraza na Jumuiya ya Wazazi wa CCM. Kilitokea wakati ambapo huduma na utumishi wake ilikuwa bado unahitajika sana na taifa hususan Bunga na Baraza la Wawakilishi na wananchi wa Jimbo la Uzini aliyekuwa anawakilisha,

Marehemu alikuwa ni mtu mwema sana, mchapa kazi hodari na muadilifu, alikuwa mzalendo na mkweli na mtiifu kwa watu aliowaongoza ambao aliwapenda na kuwatumikia kwa moyo wake wote.

Nakuomba unifikishie salamu zangu za rambi rambi kwa wajumb wa Baraza la Wawakilishi na kupitia kwako kwa familia ya marehemu, tupo pamoja nanyi katika msiba huu ni msiba wetu sote, ni mapenzi ya mola muumba wetu na kazi yake haina makosa, tuzidi kumuomba ampe mapumziko mema na ishaalla amjaalie pepo yake. Amin.

Hizo ni salamu ambazo naomba nikupeni rasmi kutoka kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya kifo cha mwenzetu Mhe. Mussa Khamis Silima.

Salamu kutoka Chama cha Mapinduzi.

Salamu nyengine za rambi rambi zilizotufikia ni salamu kutoka kwa Chama cha Mapinduzi, zinasema Mhe. Spika, wa Baraza la Wawakilishi saruku la posta 902 Zanzibar .

Barua hii ilikuwa ni ya tarehe 23/8/2011 kwa niaba ya wafanyakazi wa Afisi Kuu ya Chama cha Mapinduzi Zanzibar wanachama na wana CCM, wakereketwa na wana maskani wa Tanzania Zanzibar Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar anatoa mkono wa pole kwako wewe binafsi pamoja na Baraza lako tukufu la wananchi, kwa kuondokewa na ndugu yetu mpendwa mchapa kazi hodari na mwana mapinduzi wa kweli mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Uzini na Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia baraza lako la Wawakilishi Mhe. Mussa Khamis Silima aliyefariki dunia tarehe 23 Agost, 2011 katika hospitali ya Muhimbili jinini Dar es Salaam.

Wananchi wa Zanzibar hasa wanachama wa Chama cha Mapinduzi tumepokea kwa hudhuni na masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha muwakilishi huyo ambae pia ni Naibu Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi, tunaamini kwaba kifo chake sio tu ni pigo kwa familia yake lakini pia kwa wanachama wote wa CCM wananchi wa Mkoa wa Kusini Unguja pamoja na Taifa kwa ujumla.

Waheshimiwa Wajumbe tunaendelea na taarifa Marehemu Mussa Khamis Siliama daima atakumbukwa kutokana na bidii na moyo wa kujituma katika shughuli mbali mbali za ujenzi wa

taifa letu na kwamba wakati wowote alikuwa mstari wa mbele katika kupiga vita umasikini nchini, aidha alikuwa mpole mpenda watu, wa rika na jinsia zote hana majungu asiyeyumba na mwenye uwezo wa kupima mambo kwa kina na upeo mkubwa.

Kutokana na kifo cha muwakilishi wetu huyo tunahakikishia ndugu jamaa marafiki pamoja na familia ya marehemu kwamba Chama cha Mapinduzi kipo pamoja nao katika kipindi hiki kigumu cha huzuni na maombelezi.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi. Amin.

Barua hii iliandikwa na Naibu Katibu Mkuu ndugu Vuai Ali Vuai. Pia naomba mpokee salamu hizi za rambi rambi kutoka Chama cha Mapinduzi.

Salamu kutoka Chama cha Mapinduzi.

Salamu nyengine zinasema Spika, wa Baraza la Wawakilishi S.L.P 902 Zanzibar.

Barua hii ilikuwa ya tarehe 24/8/2011 kwa heshima ya Chama cha Mapinduzi tafadhali naomba uhusika na mada hiyo iliyopo hapo juu, uongozi wa CCM Mkoa wa Mjini Magharibi umepokea kwa huduni na majonzi kwa masikitiko makubwa taarifa ya kifo cha Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Jimbo la Uzini kupitia tiketi ya CCM, ambae pia alikuwa ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Baraza la Wawakilishi marehemu Mussa Khamis Silima.

Kifo kilichotokea tarehe 23/8/2011 kutokana na ajali ya gari iliyotokea huko Dodoma, ukweli huo ni msiba mkubwa sana kwa familia ya marehemu, Baraza la Wawakilishi, Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wananchi wa Jimbo la Uzini. Chama cha Mapinduzi, Jumuiya ya Wazazo na wananchi wote wa Tanzania.

Marehemu Mussa Khamis Silima tulikuwa tunamuelewa vyema kwa uhodari wake wa ufanyaji kazi, ushirikiano na upendo juu ya wenzake, ni mtu muelewa na mwenye busara katika kutoa uamuzi wa mambo yake, kifo chake kimeacha pengo kubwa kwa familia yake na taifa zima kwa ujumla.

Hivyo kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya uongozi mzima wa CCM Mkoa wa Mjini Magharibi hadi kufikia ngazi zote za chini yake naomba upokee salamu zangu za rambi rambi kwa kusema pole sana Mhe. Spika, kwa msiba huo ambao umeupata msiba ambao sio wako peke yako ni msiba wetu sote.

Tumuombee Mwenyezi Mungu ailaze mahali pema roho ya marehemu kumfufua akiwa miongoni mwa watu wema. Amin

Ahsate sana.

Barua hii imeandikwa kwa niaba ya Katibu wa CCM Mkoa wa Mjini Magharibi ndugu Ali. S. Suleiman.

Salam nyengine kutoka Chama cha Mapinduzi Mkoa wa Mjini Magharibi

Salam nyengine kutoka kwa Jumuiya ya Ali Yousuf

Zinasema *Honorable Pandu Ameir Kificho, Speaker of the House of Representative Zanzibar, subject condolence message. We reserved with shock the news of for sad demise of our beloved brother late Maalim Mussa Khamis Silima.*

On behalf of Sheikh Al-Youseif Foundation and on my one behalf, we tender our heartfelt condolences to you and to the rest of the aggrieved.

May Allah rest his Soul in eternal peace.

I beg to remain in solidarity.

Salam hizi zilitumwa na ndugu Omar Tarib Omar ambae ni Ofisa wa AL-Youself Foundation hapa Zanzibar.

Nakuombeni pia Waheshimiwa Wajumbe mpokee salamu hizo.

Hizo ni baadhi ya salamu lakini bila ya kusahau salamu muhimu ambazo zilikuwa ni salamu kwa njia ya simu.

Salamu kwa njia ya simu kutoka kwa Mhe. Spika, Anna Makinda.

Ambae ametupa pole kwa msiba wa Mhe. Mussa Khamis Silima, lakini kwa vifo vya watu wengi kutokana na kuzama kwa meli ya *Spice Islanders,* anatupa pole kwa misiba yote miwili mikubwa iliyotufika.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya salamu hizo na kwa sababu ya misiba hiyo mikubwa iliyowafika ndugu zetu, Mheshimiwa wetu mwenzetu lakini pamoja na wananchi mbali mbali wa Tanzania kutokana na kuzama kwa meli ya Spice Islander niombe sasa tusimame kwa dakika moja tuwaombee marehemu wote hao.

Hapa Waheshimiwa Wajumbe walisimama kwa dakika moja kwa ajili ya kuombeleza .
Mhe. Spika: Mungu awalaze mahali pema. Amin. Ahsanteni sana

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Afisi ya Rai Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Kny: Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais): Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 1 Agost, 2011.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afisi ya Rai Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kuwasilisha mezani hotuba kuhusu Ripoti tatu (3) za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Omar Ali Shehe (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC): Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) kuhusu Ripoti tatu (3) za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Kipindi cha Mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

Mhe. Waziri wa Afya: Hotuba kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali Pamoja na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Naomba kuwasilisha.

Mhe. Ashura Sharif Ali (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Naomba kuwasilisha mezani hati ya hotuba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 1

Uingizaji Wa Bidhaa Zilizotumika

Mhe. Rufai Said Rufai - Aliuliza:-

Katika miaka ya karibuni Zanzibar imekuwa kituo cha kupokea bidhaa zilizotumika kutoka nchi mbali mbali.

(a) Mhe. Waziri huoni kwamba kuendelea kupokea bidhaa hizo kunaifanya Zanzibar jaa la bidhaa chakavu.

(b) Wizara yako imejipangaje kukabiliana na changamoto hiyo kwa maslahi ya mazingira yetu na vizazi vya baadae, hasa ikizingatiwa kwamba Zanzibar ni visiwa vidogo sana.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Spika, kabla ya kujibu suala la mjumbe naomba uniruhusu nitoe mkono wa pole kwako Mhe. Spika na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi.

Lakini vile vile kwa Mhe. Spika wa Bunge la Jamuhuri la Muungano wa Tanzania pamoja na Waheshimiwa wabunge wote na familia ya marehemu pamoja na wananchi wote wa Jimbo la uchaguzi la Uzini, kwa kuondokewa na mwenzetu marehemu Mhe. Mussa Khamis Silima. Namuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahala pema Peponi. Amin.

Vile vile Mhe. Spika, naomba unipe ruhusa kutoa mkono wa pole kwa Wazanzibari wote na kwa Watanzania kwa ujumla kutokana na msiba mkubwa uliotufika, kutokana na kuzama kwa meli ya *MV. Spice Islander I*, siku ya Tarehe 10 September, 2011. Namuomba Mwenyezi Mungu azilaze roho na marehemu mahala pema Peponi. Amin.

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Rufai Said Mwakilishi wa wananchi wa jimbo la Tumbe suala lake Nam. 142, naomba uniruhusu tena nitoe maelezo machache juu ya suala hili la bidhaa chakavu (mitumba).

Mhe. Spika, suala la bidhaa chakavu ni changamoto kwa nchi zote zinazoendelea. Bidhaa hizo zinajumuisha nguo, magari, pikipiki, baiskeli, matairi, lakini pia kwenye vifaa vya *electoric* na umeme ambavyo kitaalamu huitwa *E-wastes electrical* na *electronics equipment* au kwa ufupi kwa jina la kitaalamu vinaitwa *E-wastes*. Mfano wa vifaa hivyo ni kama compyuta, televisheni, mafriji, mashine za kufulia, pasi za umeme, redio, simu na mfano wa mambo hayo.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Rais ina majukumu ya kusimamia suala zima la udhibiti wa uchafuzi wa mazingira unaotokana na bidhaa chakavu za umeme na *electronics*. Bidhaa za aina hii ni zile zilizofikia kikomo cha matumizi yake na hivyo kutelekezwa kwa kusafirishwa nje ya nchi zilipotumika kinyuma na sheria za nchi hizo na kuletwa nchini kama bidhaa zilizotumika.

Mhe. Spika, madhara ya kemikali zilizomo kwenye nyingi ya bidhaa hizo ni makubwa sana kwa afya ya binaadamu na mazingira kwa ujumla. Mfano wa bidhaa hizi hutengenezwa kwa kutumia madini makali na ya sumu *(heavy metals)* yaani kama vile *lead, mercury na cadmium.* Ambavyo kama hayajachukuliwa hadhari ya kudhibiti yasiingie kwenye vyanzo vya maji ya ardhini huweza kusababisha maradhi makubwa mbali mbali ikiwemo saratani kwa wanadamu.

Mhe. Spika, mwaka 2010 Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais kupitia Idara ya Mazingira ilifanya utafiti wa bidhaa chakavu nchini kwa ajili ya kupata taarifa sahihi za hali halisi ilivyo ili kujenga muelekeo wa baadaye wa suala hili.

Maoni ya wadau mbali mbali kutoka taasisi za serikali, watu binafsi, wafanyabiashara na taasisi za kiraia yalikusanywa na kuwa msingi wa mapendekezo hatua zinazofaa kuchukuliwa na serikali. Utafiti umeonesha kuwa katika kipindi cha miaka sita iliyopita, uingizwaji wa makontena bandarini Zanzibar ulifikia makontena 23,000 kwa mwaka. Kwa uchache asilimia 20 ya makontena yote hayo yanakisiwa kuingiza bidhaa chakavu Zanzibar kila mwaka. Ukichukua ujazo wa kontena la kawaida la futi 20 na uzito wake wa tani 21.6 hesabu zinaashiria kuwa Zanzibar inaingiza kiasi cha tani 99,360 za bidhaa chakavu za aina zote kwa mwaka ikiwemo magari, baiskeli, pikipiki, nguo pamoja na vifaa vya umeme na *electronic*.

Takwimu za Tume ya Utangazaji Zanzibar zinasema kuwa hivi sasa tume hiyo inayo hesabu ya televishen laki 3 chakabu pamoja na redio laki 980 zilizopo nchini na kwamba hakuna ufumbuzi wa kujua vipi na wapi kutakapohitajika kuzitupa bidhaa hizo chaka bila ya kuathiri mazingira ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo ya kina naomba sasa kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 142 lenye vipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Kuendelea kuingiza na kupokea kiholela bila ya kuwa na taratibu ya viwango vya biashara, afya na mazingira. Kwa bidhaa hizo basi kunaifanya Zanzibar kuwa jaa la bidhaa chakavu. Tusipokuwa na utaratibu uliowazi wa kudhibiti bidhaa hizi zisiingizwe nchini kiholela itakuwa ni hatari kwa afya zetu pamoja na mazingira yetu kwa ujumla.

Mhe. Spika, Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais katika kukabiliana na changamoto ya suala hili la bidhaa chakavu, tayari imeshaandaa kanuni za kudhibiti uingizwaji, uuzwaji na utupaji wa bidhaa hizo za umeme na electronics hapa nchini. Matumizi ya kanuni hiyo yataisaidia Zanzibar kuwa salama kutokana na madhara ya bidhaa chakavu za aina hiyo kwa faida yetu na vizazi vyetu vya baadaye. Sambamba na utekelezaji wa kanuni hiyo kutakuwa na mpango wa kuelimisha jamii juu ya athari za kiafya na makimazingira zinazoambatana na bidhaa chakavu za aina hiyo.

Mhe. Spika, naomba niliarifu Baraza lako tukufu kwamba, kanuni hiyo tayari imekwisha kamilika na Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais ipo katika hatua ya mwanzo wa kuwasiliana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika kupata maoni ya kisheria ya kiutendaji.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Spika, nashukuru sana kwa majibu marefu ya Mhe. Waziri, lakini nitakuwa na suala moja la nyongeza.

Kwa kuwa bidhaa hizi sana hupita katika maeneo mawili ya Bandarini na Uwanja wa ndege kwa kuwa maeneo hayo ndio ambapo husambaza bidhaa hizi kufika katika maeneo yetu. Je, Wizara yako Mhe. Waziri haiyoni kwamba ni bora kinga kuliko kutibu?

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, ni kweli Ofisi yangu imeliona hilo. Na kama atakuwa amezingatia zaidi katika majibu yangu tumeeleza kwamba tayari tumeandaa kanuni ambayo itadhibiti uingizwaji wa bidhaa hizo katika sehemu hizo mbazo amezitaja.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri na marefu ya Mhe. Waziri, lakini amekiri kwamba hilo ni tatizo na ni tatizo ambalo linaikumba nchi nyingi za ulimwengu wa tatu.

Je, Wizara yake kupitia Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais imeshapata eneo la kutenga kwanza hilo ili hayo yatakayofanywa baadaye yafanywe, lakini eneo la kutenge hiyo *deposit* ya eneo lipo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, kikawaida maeneo kwa ajili ya kuvikusanya vifaa hivyo huwa yanapatikana pale haja inapotokea. Lakini kwa sasa hatujaainiha hasa eneo lenyewe lipo sehemu gani na lipo wapi. Kwa sababu bado hatujaupanga ule mkakati wenyewe na kuona jisi gani sasa ni tayari tuzikusanye kwa ajili ya kuweza kuziharibu. Kwa sababu kuziharibu bidhaa hizo si suala la mara moja ni suala la kitaalamu na ni suala linalohitaji fedha nyingi. Pia tunategemea utaalamu wa wenzetu wa nchi zinazoendelea.

Mara ya mwisho bidhaa za aina hizo na takataka za sumu zilibidi ziondoshwe hapa nchi kwetu visiwani pamoja na Tanzania kwa kuletwa meli na baadaye zikasafirishwa takataka hizo ili kupeleka sehemu ambazo wao wanaweza kuziharibu bila ya uharibifu wa mazingira na kuleta uharibifu kwa binaadamnu.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Nakushukuru sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Waziri suala la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri aliyojibu.

Amekiri kwamba sasa hivi zimejaa bidhaa hizo ambazokuwa zinasababisha madhara kwa wananchi. Wakati huo huo sasa hivi bidhaa hizo zinaendelea kuingizwa.

Je, kwa sababu wana mpango wa kuziangamiza zile ambazokuwa zimeshaingizwa na je, kwa sababu wananchi wanaendelea kuziingiza Wizara yake ina mpango gani wa dharura wa kuzuia kuingizwa tena bidhaa hizo ili zisiongezeke tena zaidi.

Mhe. Waziri wa Makamo wa Kwanza wa Rais: Mhe. Spika, anayoyazungumza ni kweli na sisi tumejipanga katika kushughulikia kuona kwamba bidhaa hizo chakavu haziendeleo kuingizwa nchini. Na ndio pale nilipozungumzia suala zima la kwamba Wizara tayari imeshaandaa kanuni ambayo itahusisha uingizwaji, uuzwaji na utupaji wa bidhaa hizo chakavu.

Ninachotaka kumuhakikishia Mhe. Mjumbe kwamba tabia ya wananchi wetu tunaielewa sana, mara nyingi watu wanapozoea jambo si rahisi kuliacha kwa mara moja. Tunahitaji mkakati wa kisheria na ndio maana tumeona tuje na kanuni ambayo sasa itakuwa ni sheria ambayo itasimamia uingizwaji wa bidhaa hizo. Si rahisi moja kwa moja kuweza kuwazuia watu usipokuwa na sheria. Lakini tutakapokuwa na sheria na kanuni ambayo imeeleza wazi wazi, basi ni rahisi kwetu sisi kama serikali kuweza kudhibiti uingizwaji wa bidhaa hizo chakavu.

Nam. 5

Msongamano Mkubwa Katika Njia ya Marikiti – Darajani

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Kumekuwa na msongamano mkubwa wa watu na magari maeneo ya Marikiti – Darajani kiasi kwamba inawachukuwa watu muda mrefu kuweza kukatisha njia kutokana na msongamano huo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuondosha tatizo hilo.

(b) Kwanini Serikali isiondoshe Kituo cha Daladala kilichopo hapo Darajani ambapo sasa panaonekana kuzidiwa na kuwekwa pahala pengine muafaka zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi - Alijibu:-

Mhe. Spika, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 5 lenye sehemu (a)na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Ni kweli kumekuwa na msongamano mkubwa wa watu na magari mbele ya soko la Darajani. Hali hii inakuja kutokana na ongezeko la vipando vya moto na pia ongezeko la idadi ya watu. Nafikiri Mhe. Mwakilishi atakubaliana name kwamba ongezeko hili la vipando vya moto na idadi ya watu katika eneo la Darajani limetokana na hakati nyingi za soko na biashara kukua kwa ujumla katika eneo hilo na mitaa iliyokaribu na jirani na eneo hilo.

Mhe. Spika, vile vile msongamano huo katika eneo hilo, umekuja kutoka na eneo hilo kuwa kituo kikuu cha usafiri wa abiria kwa gari za mashamba, ikiwemo Mkwajuni, daladala na TAX. Pia wafanyakazi wetu wa Afisi mbali mbali za Serikali na wanafunzi wanakitumia kituo hicho kwa kupata usafiri wa kuondokea baada ya kukamilisha kazi zao za kila siku na masomo kwa wanafunzi. Hata wananchi wa kawaida wanakitumia kituo hicho kama kituo chao kikubwa cha kufikia na kuondokea kwa usafiri wan chi kavu kwa mjini na mashamba hapa Unguja kama nilivyosema hapo awali.

(a) Mhe. Spika, kuondosha tatizo liliopo Serikali inachukua juhudi za kuimarisha matumizi gora ya alama za barabarani ikiwemo zile za kuvukia njia kwa watembeao kwa miguu, pia kutoweka gari au kutoegesha gari sehemu zisizoruhusiwa. Vile vile kutopitisha gari katika sehemu zisizoruhusiwa.

(b) Kwa sasa serikali haina mpango wa kukihamisha kituo hicho cha daladala. Suala la msingi ni watu wote wenye vipando vya moto kufuata taratibu zilizowekwa za alama za barabarani na kuwafikiria watumiaji wengine wa barabara katika eneo hilo wanaokwenda kwa miguu hasa walemavu, watoto wadogo, watu wazima na wanafunzi.

(c) Mhe. Spika, hata hivyo serikali inalitafakari wazo la kutafuta eneo mbadala kama kituo chengine cha daladala.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Waziri umezungumza kwamba kuna juhudi kubwa serikali inayofanya kuhusu alama za barabarani. Kumekuwa kuna kilio kikubwa cha wananchi wanaokaa mtaaa wa Mchangani kuvuka barabara kuelekea Chuoni mbele ya Baraza lako la Manispaa. Ni muda mrefu sasa wananchi hao hawajajibiwa na kuna hatari kupoteza maisha ya watoto. Sijui umelionaje suala hili?

Mhe. Spika: Hebu tubaki kwenye eneo la Darajani pale. Sasa fanya utaratibu ili

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Spika, alitaja kuhusu juhudi ya Serikali kuhusu alama za barabarani.

Mhe. Spika: Hebu niandikie suala la msingi suala lako.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa ya kuuliza suali dogo tu la nyongeza.

Kwa kuwa ni ukweli usiofichika kwamba kituo cha daladala kilichokuwepo Darajani, kimeshazidiwa na watu pamoja na magari tena magari chakavu kama tulipopata jibu sasa hivi kutoka kwa Mhe. Waziri. Na kwa kuwa mpango madhubuti haujakamilika wa kuyadhibiti magari chakavu bado yanaendelea kuingia tena kwa kasi kubwa. Jambo ambalo yanaendelea kuzua tatizo kubwa katika kituo kile cha Darajani.

Kwa kuwa kuna ardhi ambayo sasa hivi haitumiki ambayo nina wasi wasi ambapo patakuja kujengwa bostani. Je, isingekuwa vyema kwa serikali kuangalia ule uwanja wa pale Maisara kumpa muwekezaji akaudhibiti vizuri halafu kikawekwa kituo cha daladala ikawa tumewekeza katika upande huo.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, kama nilivyosema kwamba nakiri kwamba msongamano mkubwa upo. Lakini kama nilivyosema pale watumizi wote kama tukifata taratibu basi msongamano ule utapungua.

Kubwa liliopo wengi hatufati taratibu, utakuta wengine tunapaki magari ambapo sehemu ambazo haziruhusiwi. Wengine zile *zebra crossing* baada ya kusimama ukapisha watembeaji kwa miguu hatusimami. Wengine tunakuwa watanja tunataka ku- *over take*. Suala la msingi kwanza tuzifate zile kanuni zilizowekwa pale. Hiyo ni kawaida miji yote pale Darajani ndio *city center* na *city center* yoyote ile ndio hali halisi.

Suala lako la msingi la magari chakavu kweli nakubaliana na *observation* yako. Magari mengi yanayoingizwa nchini ni machakavu na hatujui yanapita vipi, lakini ndio yanaingia. Hili kama serikali tunalichukua ili tulifanyie kazi Wizara yetu pamoja na Wizara husika tuweze kuyadhibiti haya magari mengine.

Suala la bustani hili ni master plan ya mji na hasa maeneo yale na ile pia inajumuisha utanuzi wa maeneo ya kuegesha magari. Kwa hiyo kituo kitasogezwa na ramani lipo pale, mtu unaweza ukenda ukalisoma na ukaliona vizuri lilivyo. Tushirikiane kuutekeleza ule mpango uliokusudiwa katika eneo lile. Ahsante.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza napenda kutoa pongezi zangu kwa kile kituo cha daladala kuwekewa lami katika kipindi kilichopita na kurahisisha utatatibu wa daladala kuingia na kutoka.

Namuuliza Mhe. Waziri je, kazi zetu tunafanya kwa kushtukizia na hakuna utaratibu wa kufuatilia tena baada ya kwisha kutekelezwa ile kazi. Kwa sababu nyuma ya kituo kile kwenye njia inayopitia Donge au Baclay sasa hivi inaitwa, kule kuna mashimo makubwa na bado hakujashughulikiwa chochote na yale mashimo yanaendelea kuila ile njia.

(a) Je, Wizara yako haina utaratibu wa kufatilia ikishajenga.

(b) Na lini unatuhakikishia kwamba eneo lile litarudishiwa lami ili utaratibu wa usafiri uendelee kama kawaida.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Kwanza tunakushukuru sana kwa pongezi ulizozitoa kwa matengenezo ya kituo kile cha daladala. Sote tunakumbuka hali ilivyokuwa zamani pale. Sote tulikuwa tunaona tabu hata kupita, lakini leo kuna mipango mizuri na gari zinateleza.

Kweli nakiri na nampongeza sana Mhe. Rashid, mara nyingi humkuta njiani hutaka kumpa lifti lakini hataki lifti yangu anakwenda kwa miguu. Kumbe akenda kwa miguu ana *observe* kila kitu anachokiona. Ni kweli nakiri mashimo yapo, na unajua hasa wakati wa mvua kama huu mashimo yale huwa yanazidi. Ni jukumu letu Baraza la Mji kushirikiana pamoja na Wizara ya Miundombinu kuweza kuyaziba mshimo yale. Namuoahidi Mhe. Rashid kwamba eneo lile na maeneo mengine ambayo yapo matatizo kama hayo tutashirikiana na wizara pamoja na mfuko wetu wa barabara ambayo unadhamana hiyo ya matengenezo ya barabara kama zile kuweza kuyashughulikia ipasavyo. Sio kama tuna mipango ya kushtukizia. Kuna Master Plan kubwa kabisa ya mji na hiyo ndiyo dira yetu kuweka mji wetu katika mazingira yanayotakiwa.

Nam. 25

Upatikanaji wa Vyeti Vya Kuzaliwa Kwa Wakati.

Mhe. Hassan Hamad Omar : Aliuliza:-

Moja kati ya vipaumbele ambavyo uliahidi mara baada ya kuteuliwa Uwaziri ni kwamba; utahakikisha hakuna usumbufu wa kupatikana vyeti vya kuzaliwa Unguja na Pemba na kwamba vyeti hivyo vitapatikana si zaidi ya wiki mbili. Lakini kuna tetesi kwamba inachukua hadi mwaka mzima mhusika hajapatiwa cheti hicho.

(a) Je, hali hiyo inasababishwa na nini.

(b) Je, lini wananchi wa Zanzibar watapata huduma hiyo kwa muda mfupi kama ulivyoahidi.

Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria: Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi suali lake Nam. 25 kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba moja kati ya vipaumbele nilivyoahidi ni kuhakikisha kuwa hakuna usumbufu wa kupatikana kwa vyeti vya kuzaliwa Unguja na Pemba na kwamba vyeti hivyo vitapatikana si zaidi ya wiki mbili. Wizara yangu imo katika utekelezaji wa azma hii kwa kutekeleza mikakati ya mabadiliko ya muda mfupi, wa kati na mrefu.

Mhe. Spika, katika jibu langu nililolitoa katika suala Nam. 127 la tarehe 24/6/2011 niliorodhesha matatizo mengi yaliyosababisha kuchelewa kupatikana kwa haraka vyeti vya kuzaliwa. Matatizo hayo ni pamoja na Upungufu wa wafanyakazi Wilayani, Upungufu wa kupata vyeti, kutokuwa na udhibiti wa kutosha wa wafanyakazi Wilayani na ucheleweshaji wa Kupelekwa kwa "*returns*" Wilayani. Baadhi ya hatua tumeshazichukua na ndio maana baadhi ya maeneo ni kweli vyeti vya watoto wanaozaliwa, na hasa Hospitali, sasa havichukui muda mrefu.

Mhe. Spika, kwa sababu bado matatizo niliyoyaelezea huko nyuma hayajatatuka yote, basi ni kweli maeneo mengine vyeti vinachelewa kupatikana. Ni kweli pia kuwa matatizo hayo zamani yalikuwa mengi sana, na ndio maana vyeti vilichukua zaidi ya mwaka kuvipata. Hivi sasa tumejaribu sana kulipunguza tatizo hili; na ninaamini kuwa tatizo hilo litamalizika karibu sana.

Mhe. Spika, naomba kulihakikishia Baraza lako Tukufu kuwa wizara yangu inayodhamira ya dhati ya kuwapunguzia wananchi adha ya kufuatilia vyeti kwa muda mrefu. Tayari mabadiliko yameanza kuonekana katika Wilaya ya Magharibi, Mjini, Micheweni, Kaskazini B na Kusini Unguja ambapo huduma za vyeti zinafanyika kwa wakati muafaka, ingawa matatizo ya hapa na pale bado yapo.

Wizara yangu imo katika hatua za kuimarisha Mifumo ya Usajili wa Vizazi na Vifo, jambo ambalo tunaamini litapunguza ucheleweshaji wa vyeti. Aidha marekebisho ya Sheria ya Vizazi na Vifo, Ndoa na Talaka,na kufanya Sheria moja , ni moja wapo ya hatua zinazokusudiwa kuchukuliwa ili kupunguza usumbufu wa upaatikanaji wa vyeti.

Mhe. Spika, wizara yangu imo katika hatua za kuona namna ambavyo Taasisi za Usajili zinaweza kushirikiana na Afisi ya Mrajis Mkuu wa serikali, ili kuweka mfumo wa usajili mwingine wowote unaomhusu mtu au mali yake katika maisha yake yote. Taratibu hizi zinatumika katika nchi za wenzetu kama vile Sychelles na Norway na zimeleta mafanikio makubwa sana. Tumeshaanza kusoma utaratibu huu kwao utaratibu huu na baada ya hapo sisi tutaishauri serikali namna gani ya kuchukua utaalamu huo ili na sisi tuweze kuutumia haraka iwezekanavyo.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nafikiri atakubaliana na mimi kuwa kuna watoto waliozaliwa tarehe 13/12/2009 na mpaka leo bado hawajapatiwa cheti.

(a) Je, ni jambo gani hasa linalosababisha kutokutekelezeka kwa ahadi zako.

(b) Mhe. Spika, namuuliza Mhe. Waziri wazee waliofikia umri wa miaka 50–70 unakumbuka kwamba hawana vyeti vya kuzaliwa lakinikunakuwa na mzungumko mkubwa na gharama kubwa ya kuweza kupata vyeti hivyo. Je, Mhe. Waziri serikali

kupitia wizara yako ina mpango gani wa kuweza kuwapunguzia kadhia hiyo wananchi wetu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kama nilivyosema mwanzo kama hasa kwa Wilaya ya Wete kwa Pemba na Wilaya ya Kaskazini "A" kwa Unguja ndizo Wilaya ambazo zilikuwa na matatizo mengi sana na tumejaribu kuyapunguza mengi. Mhe. Spika, hili ni kweli kwamba katika Wilaya hizi kwa mfano Wilaya ya Kaskazini "A" kuna vyeti hata miaka 3 mtu alikuwa hajapata cheti cha kuzaliwa.

Mhe. Spika, ni kwamba tumejaribu kwa uwezo wetu wote kuhakikisha kwamba matatizo hayo yametatuka. Ni kweli kwamba hilo tumelifanya na hivi sasa wengi wameshapata vyeti vyao isipokuwa kuna baadhi kutokana na matatizo hayo hayo ya nyuma bado tunajaribu kuyatatua ili waweze kupata vyeti vyao.

Mhe. Spika, kama nilivyosema ni kwamba tumechukua hatua sasa hivi kwa mfano, tumejaribu kupeleka watu wetu kutoka wizarani katika wilaya hizi ili na wao wawepo pale kuhakikisha kwamba vyeti vinapatikana kwa haraka. Pia tumehakikisha kwamba wafanyakazi wanaohusiana na suala la uandikishaji wa vyeti hawapelekwi kufanywa shughuli nyengine hilo lilikuwa ni jambo moja ambalo linachelewesha vyeti. Kwa hivyo, hatua hizi bado tunazichukua na kama walivyosema kuwa bado Wilaya ya Wete na Wilaya ya Kaskazini "A" ni matatizo sugu ambayo yapo kwa hiyo tutajitahidi kuyatatua matatizo hayo haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, kwa upande wa pili suala la wazee wanaoazia miaka 50-70 na hawana vyeti hili ni suala letu la *registration* kuna utaratibu wake uliowekwa ni kwamba unachukua fomu, na fomu hiyo unaijaza. Mhe. Spika, katika kujaza fomu hiyo unapitia taratibu zake ikiwemo Kamati ya Sheha ya pahala ambapo unaishi, Mkuu wa Wilaya halafu Mahakamani ili kwa kula kiapo. Baada ya kufanya yote hayo fomu hiyo inakuja Afisini kwa Mrajisi na yeye baada ya kuhakikisha kwamba yote hayo yametekelezwa ndio anaweza akatoa cheti cha kuzaliwa baada ya malipo ya ada ambayo imewekwa.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

a) Mhe. Spika, tokea mapinduzi ya mwaka 1964 wizara hii inayohusika na kutoa vyeti vya watoto imekuwa ikitumia *typewritters* ambazo hazikuwa nzuri na matokeo yake vyeti vya watu wengi vilikuwa vina makosa ambayo kwa mfumo wetu wa kisasa wa *computerization* vyeti vile vinakuwa havikubaliki kutiwa katika mfumo wa *computer*, jambo ambalo limesababisha usumbufu mkubwa wa wananchi.

   Je, Mhe. Waziri wizara yake ina mpango gani wa kuwapunguzia mzigo wananchi kwa sababu kuna wananchi wengi ambao wamekosa haki zao kutokana na makosa yaliyomo katika vile vyeti.

b) Mhe. Spika, ni kwamba ukichukua hatua kwenda kufanya marekebisho ya cheti chako kunakuwa na ada na mara nyengine haiwi ndogo. Kwa mfano, ukienda kubadilisha cheti chako unalazimika kulipa shilingi 7000/= au mara nyengine zaidi.

Je, Mhe. Waziri ana mpango gani kuhakikisha kwamba kwa sababu makosa haya hawakuyafanya wananchi wenyewe ni *typewritter* zao ambazo ni mbaya, hivyo ana mpango gani wa kuhakikisha marekebisho haya yanafanywa bila ya malipo.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, kwanza naomba radhi kwamba sikusikia vizuri lakini nitajaribu kujibu kwa kadri nilivyosikia kama sivyo naomba anisamehe.

Mhe. Spika, kuhusu suala la kwanza ni kwamba kweli vyeti vyetu vina matatizo katika kupiga *type* na hilo tumeshaliona, nafikiri miezi miwili iliyopita nyuma tulikaa tukalizungumza suala hili katika ofisi zetu. Mhe. Spika, ni kwamba tuna mpango sasa kwamba vile vyeti vitolewe katika kompyuta ili cheti kiwe kina kinasomeka vizuri, lakini nayo ina matatizo kwa sababu vyeti hivi ni muhimu sana. Mhe. Spika, ni kwamba tunajua matatizo ya kompyuta watu walivyo watundu katika IT ukikiweka pale kinaweza kikatolewa kwa hivyo ukapata vyeti vingi na ukawapa watu wengi ambao hawahusiki. Kwa sababu vikiwemo kwenye kompyuta wao huwa wanatoa tu kwa hiyo inaweza ikatuletea matatizo baadae.

Mhe. Spika, ni kwamba tumejaribu kushirikiana na wataalamu wa mambo haya ya IT ili kuwe *mark* maalum katika vyeti vile ambavyo hata mtaalamu mwengine hatoweza kuitia ile mark ambayo inatoka katika Afisi ya Mrajis. Kwa hivyo, tukishakufanikiwa hilo hivi sasa wamo katika kazi na hapo tutapunguza hata ucheleweshaji kwa sababu lile suala la kuchapa vyeti kutoka *Government Press k*uja afisini halafu ikaandikwa kwa kompyuta za zamani itakuwa halipo. Lakini naomba mtupe muda kidogo kwa sababu hili tukiharakisha linaweza likatutia hasasa baadae.

Mhe. Spika, suala la pili ni kwamba makosa haya yanapotokea ni kweli mtu anapopewa cheti huwa anachukua tu hasomi, akishakufika nyumbani wakati anataka kukitumia kile cheti anaona kwa mfano Said hamna "I". Kwa hivyo, akirudi itakuwa ni kosa kama analipishwa na kama kuna watu ambao wanafanya hivyo ikiwa ni makosa ya idara yetu basi atafanyiwa bure, lakini ikiwa kuna suala la kubadilisha jina hilo itabidi alipe. Mhe. Spika, kwa wale ambao wana makosa kama hayo na wanalipishwa naomba watuone ili tuweze kuwarekebishia bila ya malipo yoyote. Lakini ikiwa mtu anataka kubadilisha jina au kubadilisha maneno mengine katika cheti hiyo itabidi alipe.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa sababu Wilaya ya Wete kuna tabu kubwa sana ya kupatikana vyeti vya kuzaliwa watu wengine inabidi kuja Unguja kuja kufuatilia vyeti hivyo. Mhe. Spika, jambo la kusikikitisha ni kuwa hata zile kumbukumbu sisi kule Pemba tunaita "vishina" ambavyo vikimaliza huletwa huku Unguja mpaka leo bado havijaja na hupata usumbufu mkubwa sana.

Je, Mhe. Waziri atasaidia vipi kuona kuwa vile vishina vinavyotakiwa kuja huku vinakuja mapema ili tupunguze usumbufu huu wa kupata vyeti hivyo vya kuzaliwa kwa watoto wetu.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, ni kwamba tunapoandikisha vyeti katika kila Wilaya ni kuwa sehemu ya vyeti vile vinabakia katika afisi zetu, na kwa wilaya nyengine isipokuwa hapa Mjini kumbukumbu zile baada ya muda zinaletwa katika afisi kuu ili kuwekwa katika *archives* na ndio maana mtu kama akipoteza cheti chake ikiwa anajua ile namba akija

katika ofisi kuu anaweza akapata cheti hicho. Kwa hivyo, kuna muda maalum ambao vishina vile vinatoka katika eneo moja kuja katika Makao Makuu. Mhe. Spika, kwa hiyo muda huo kama haujafika vyeti vile au kumbukumbu zile zinabakia kule. Lakini ukipita tu ni kwamba kumbukumbu zile zinakuja afisi kuu.

Mhe. Spika, mimi nasema tutashauriana na wenzangu ili tutizame uwezekano ama wa kue-*stand* kumbukumbu zile lakini pia kuna hatari kwa sababu katika maofisi yetu hakuna pahala pazuri pa kuhifadhi zinaweza zikaharibika na zikiharibika itakuwa tumeshakosa kumbukumbu za kitaifa. Lakini hilo ni suala la kulifanyia kazi na kutizama na kujua namna gani tunaweza tukasaidia hali kama hii.

Nam. 9

Ujenzi wa Barabara

Mhe. Salim Abdalla Hamad - Aliuliza:-

Kampuni ya *MECCO* ambayo imeteuliwa kujenga barabara ya Konde – Wete na Gando – Wete imeshaanza kazi ya ujenzi wa barabara hizo.

(a) Je ni muda gani tokea Kampuni hiyo imeanza ujenzi wa barabara hizo na ni hatua gani kila barabara imeshafikia.

(b) Tunatarajia kazi hiyo kumalizika lini.

(c) Barabara kongwe ya Wete – chake, nayo imo katika mpango wa kujengwa. Je, kampuni gani imepewa kazi ya ujenzi wa barabara hiyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 9 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:
Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo.

Mhe. Spika, mradi huu wa barabara aliyoulizia Mhe. Mwakilishi ni mradi wa barabara unaojumuisha ujenzi wa barabara tatu Chake – Wete, Wete – Konde na Wete – Gando/Raha - Ukunjwi zenye urefu wa km 52.1. Mradi huu unafadhiliwa na *BADEA* na *SAUD FUND* ikishirikiana na SMZ, na unajengwa na kampuni ya Mwananchi *Engineering & Construction (MECCO)* kutoka Dar-es- Salaam ikisimamiwa na kampuni ya *J. Burrow* kutoka Afrika Kusini. Mradi huu umegawika katika *Phase* mbili kama ifuatavyo:

Phase 1: Barabara za Wete – Konde na Wete – Gando.
Phase 2: Barabara ya Chake – Wete.

Kazi inayoendelea sasa hivi ni *Phase 1* na ilipangwa kukamilika ndani ya miezi 29 na ilianza rasmi tarehe 01/09/2009 kwa barabara ya Wete – Konde ikifuatiwa na barabara ya Wete – Gando ambayo ilianzia Julai 2010. Hivyo *Phase 1* inatakiwa kukamilika tarehe 31 Januari 2012. Mhe. Spika, napenda nikiri mbele ya Baraza lako tukufu kwamba inawezekana muda huo tulioutarajia ukapita bila ya barabara hizi kukamilika.

Baada ya maelezo hayo naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

(a) Kampuni imeanza ujenzi wa barabara hizo rasmi tarehe 01/09/2009 kwa barabara ya Wete - Konde ikifuatiwa na barabara ya Wete – Gando ambayo ilianzia Julai 2010. Hatua iliyofikiwa ya kila barabara ni kama ifuatavyo:-

Barabara ya Wete – Konde (14.9 km) maelezo yake ni kama ifuatavyo:-

Hatua iliyofikiwa ni uwekaji wa kifusi wa tabaka la pili (*sub base*) kwa urefu wa 13km ambayo ni sawa na asilimia 85%. Kazi iliyobakia ni kumalizia km 2 za *sub base*, kuweka tabaka la tatu la kifusu (*base*) na uwekaji wa lami pamoja na ujenzi wa daraja 1.

Barabara ya Wete – Gando/Raha – Ukunjwi (15.1km).
Barabara ya Wete - Gando (11.4).

Hatua iliyofikiwa ni usafishaji wa barabara urefu wa 8.5km pamoja na kutengeneza tuta la barabara lenye urefu wa 3 km.

Barabara ya Raha – Ukunjwi (3.6 km)

Hatua iliyofikiwa ni usafishaji urefu wa 3 km.

(b) Kazi hiyo inatakiwa ikamilike tarehe 31 Januari 2012 kwa phase ya kwanza kwa mujibu wa mkataba.Lakini hata hivyo yawezekana muda huo ukawa hautoshi pasi na kazi hiyo kukamilika.

(c) Mhe. Spika nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba barabara kongwe ya Wete – Chake nayo imo katika mpango wa kujengwa. Barabara ya Wete -Chake ni moja kati ya barabara tatu katika mradi wa ujenzi wa barabara tatu za Kaskazini-Pemba unaofadhiliwa kwa pamoja baina ya *BADEA,SOUD FUND* na SMZ.Barabara nyengine ni Wete- Gando na Wete-Konde.Ujenzi wa barabara hizo unatekelezwa na *MECCO*. Ujenzi huo umegawika katika awamu mbili:-

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Tukiangalia takwimu aliyoitoa Mhe. Naibu Waziri aliyoitoa ni kwamba barabara hizi zimechukua siku nyingi sana na mpaka leo ndio kwanza hazijamalizika. Kwa mfano, kama ile barabara ya Gando-Wete tokea mwaka 2009 na halafu ni kampuni hii hii nasikia

iliyopewa kutengeneza barabara ya Wete-Chake Chake. Je, Mhe. Naibu Waziri miaka mingi itapita watu bado wamo katika usumbufu kwa kutumia kampuni hii, hivyo hakuna uwezekano wa kubadilisha mikataba. Kwa mfano, *PRISMO* ambayo ilikuwa inafanya kazi Pemba tulizungumziwa hivi hivi sana lakini mwisho ikabidi ifukuzwe hapa Unguja.

b) Mhe. Spika, katika utengenezaji wa barabara ya Konde-Wete kulikuwa na watu waliothirika kwa kuvunjiwa majumba yao kwa sababu ya barabara ile ilipopita. Lakini kuna watu 10 wa Kinyasini walifikwa na kadhia hiyo katika utengenezaji wa barabara na tukafuatilia tukachukua majina na sahihi ya Sheha kwamba suala hili ni kweli tukampelekea Mhe. Waziri na mwisho wake waliahidiwa kulipwa. Je, wale watu 10 walioathirika ambao wengine wameyahama majumba yao wameshapewa fidia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, kama tulivyoeleza katika maelezo ya awali ni kwamba barabara hizi huenda zikachelewa kumalizika kinyume na mkataba au tofauti na tarehe iliyokusudiwa katika mkataba. Lakini ni kwamba sababu zipo nyingi kwa upande wetu sana serikali na kwa upande wa mjenzi, tunaendelea kuzungumza na mjenzi kuona kwamba anajitahidi kukamilisha barabara hizi kwa kuzingatia muda, mahitaji na malengo ya serikali katika kufanikisha maendeleo kwa wananchi wake.

Mhe. Spika, mategemeo yangu ni kwamba atakapoweza kukamilisha kazi hii ni kwamba kuna faida kubwa tutakayoipata wananchi kulikoni itakapoamua serikali kuvunja mkataba na kuanza utaratibu mpya wa kutafuta mkandarasi.

Mhe. Spika, ni kwamba nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba kuna wananchi ambao wameathirika katika ujenzi wa barabara hii na kama nilivyosema katika maelezo yangu ni kuwa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tumejenga utaratibu wa kwamba hatutavunja nyumba ya mtu katika ujenzi wa barabara kabla ya kumlipa fidia. Mhe. Spika, analoliulizia Mhe. Mwakilishi ni nyumba ambazo zimeathirika katika harakati za ujenzi wa barabara, napenda nilithibitishie Baraza lako hili tukufu na Mhe. Mwakilishi kwamba tayari timu ya watendaji wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano imeshafanya tathmini, fedha zimeshapatikana na muda wowote kuazia wiki inayofuata watu hawa watalipwa fidia.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii kumuuliza maswali madogo Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Spika, tunashukuru kwa majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri namna ya kampuni hii inavyoendesha ujenzi wa barabara hizi na ule muda ambao waliotegemea kumalizia.

Mhe. Spika, kampuni hii kabla ya kupewa barabara za kule Pemba ilipewa barabara ya Kiembesamaki-Fumba baadae ikapewa na barabara ya Amani-Dunga, baadae kampuni hiyo hiyo ikapewa barabara ya Mfenesini-Bumbwini na baadae kampuni hiyo hiyo ikapewa barabara ya Wete-Konde, na baadae kampuni hiyo hiyo ikapewa barabara ya Wete-Gando pamoja na hiyo nyengine.

Mhe. Spika, katika historia kampuni hii waliiahidi serikali na wananchi waliambiwa kwamba barabara ya Amani-Dunga na Bumbwini-Mfenesini ingelimalizika mwezi wa Septemba, 2010 kabla ya uchaguzi. Tulitegemea kabla ya kwenda katika uchaguzi barabara hizi zingelikuwa

zimeshamaliza, lakini mpaka hivi sasa Mhe. Spika, barabara ya Amani-Dunga haijamaliza, barabara ya Mfenesini-Bumbwini haijamaliza na sasa hivi Mhe. Waziri anatwambia kwamba barabara zile za Pemba zinategemea kumaliza katika kipindi hiki.

Je, suala langu liko hapa ni kwamba hatuoni mpaka sasa hivi kwamba kampuni hii haina uwezo wa kufanya kazi zote ambazo tulizowapa na serikali kabla ya kuingia hasara zaidi, hatuoni kwamba kampuni hii ikanyanganywa baadhi ya barabara hasa hizo za Pemba kwanza wakamaliza hizi za Unguja halafu baadae hizo za Pemba wakapewa kampuni nyengine.

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii kukazia majawabu ambayo ameyatoa Mhe. Naibu Waziri, lakini vile vile kujibu swali la Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Spika, serikali huwa ina mikataba na mjenzi na kama kuna sababu za msingi ambazo zinamuelemea mjenzi na kwamba pengine serikali hawana sababu na wao zilizosaabisha mjenzi huyo kuwa na sababu zile za kuvunja mikataba, nakubaliana naye kabisa kwamba serikali inaweza ikamwita mjenzi ikamsomea madhambi yake na kwa mujibu wa mikataba ilivyo na ikionekana kweli kwamba mjenzi ana makosa zaidi mkataba huo ukavunjwa. Lakini kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri kwamba mikataba ina pande nyingi, hizi barabara ambazo tunazungumzia za Pemba ni kwamba kuna sehemu 3. Kuna Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar nao wana majukumu yao kulipa fidia, kuondoa vikwazo katika barabara na kumpa mjenzi uwanja kabisa ambao hauna matatizo. Hilo liangaliwe kwanza.

Vile vile kuna huyu ambaye anatusaidia kwa njia ya mkopo yeye anakamilisha vifungu vyote kama vilivyo katika mikataba. Kwa hivyo, na mkandarasi na yeye pia ana majukumu yake kama sehemu zote hizi tatu hazikufanya kazi kwa mujibu wa mkataba inakuwa ni vigumu kusema serikali huyu hana uwezo, huyu ana uwezo kwa hivyo huyu tumnyanganye. Kwa hivyo, lililopo hapa Mhe. Spika, ni hizi sehemu tatu kila mmoja kujua majukumu yake na kwamba kila mmoja ametimiza majukumu yetu kwa mujibu wa mkataba. Naomba nilitaarifu Baraza hili kwamba hivyo sivyo ilivyo, ni kwamba tuna mapungufu yetu serikali na ni kwa sababu ya uwezo tulionao kuna mapungufu ya mlipaji na ni kwa sababu za *procedure* za mlipaji, na bila shaka mkandarasi na yeye anachukua nafasi hiyo kwamba hili na hili hamjakamilisha, na kama yeye hana uwezo basi anajifichia hapo. Mhe. Spika, lakini mimi si shauri kwamba wakati umefika wa mkandarasi huyu kusema hana uwezo labda pengine serikali ikaamua kumwita na kuvunja huu mkataba, hivyo hasara itakuwa kubwa kuliko tijara.

Mhe. Spika, mimi nilitaka kufafanua hayo kwa ufupi.

Nam. 3

Mikato ya Wajibu kwa Walimu

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa - Aliuliza:-

Inasemekena kwamba walimu wa Zanzibar wanaongoza kwa kukatwa mishahara yao kupitia mwajiri wao WEMA. Kuna kile kinachoitwa mchango minne ya wajibu ambapo walimu

hulazimika kukatwa Tsh 4000/= chini ya usimamizi wa walimu wakuu. Michango hiyo ni kwa ajili ya:-

(i) Tamasha la elimu bila ya malipo
(ii) Siku ya walimu duniani
(iii) Elimu ya watu wazima
(iv) Fedha kwa ajili ya vituo vya walimu TC

Aidha, kuna baadhi ya Wilaya kama vile Mkoani huwakata walimu asilimia 2% ya mshahara , Wilaya ya Micheweni hukata Tsh 500 kwa ajili ya Skuli za Maandalizi wakati Wilaya ya Kusini kuna mchango wa ujenzi wa Makao Makuu ya Wilaya. Kwa kutilia maanani kwamba walimu ni kundi kubwa la wafanyakazi na kwa idadi ya sasa ni kama1200 na fedha hizo zinakusanywa na WEMA kupitia michango hiyo ya wajibu ni mamolioni kwa mwaka, ambazo husimamiwa na wizara moja kwa moja.

(a) Mhe. Waziri ni kiasi gani cha fedha kilichokusanywa na Wizara kupitia michango wanayolazimishwa walimu kwa miaka mitano iliyopita.

(b) Ni mamlaka gani iliyowasilishiwa mahesabu ya fedha hizo kwa ajili ya kuhakiki usahihi wa matumizi yake, kwa vile hazijaonekana katika taarifa za Bajeti za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

(c) Mhe. Waziri atalieleza nini Baraza kuhusu tuhuma za kuwa matumizi ya fedha hizo hayawasilishwi kwenye chombo chochote na kuwa maofisa waandamizi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wamekuwa wakitumia fedha hizi za umma bila ya kufuata taratibu na kanuni za matumizi ya uuma.

(d) Je, mpaka lini wizara yako itaendelea na mpango wake wa kuwakata walimu fedha zao bila ya ridhaa na utashi wao, na kwa nini fedha hizo zisipatikane kwenye Bajeti ya Wizara badala ya kuwachangisha walimu.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali -Alijibu:-

Mhe. Spika kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 lenye sehemu (a), (b) na (c) na kwanza naomba kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Ni kweli kuwa walimu na wafanyakazi wengine wa wizara wanachangia shughuli mbali mbali za kielimu ikiwemo sherehe za Tamasha la Elimu Bila ya Malipo. Siku ya Walimu Duniani, Juma la Elimu ya Watu Wazima. Pia walimu huchangia fedha kwa ajili ya uendeshaji wa vituo vya walimu. Wizara inapongeza sana kwa michango yao, hata hivyo, michango hiyo ni ya hiari na wala fedha hizo hazikatwi katika vocha ya mshahara.

Kuhusu dhana ya kuwa walimu kukatwa asilimia 2 ya mshahara wao kwa skuli za Wilaya ya Mkoani na shs. 500/- kwa skuli za Wilaya ya Micheweni kwa ajili ya skuli za maandalizi. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa kwamba michango hiyo haipo kabisa na wizara haijawahi kukusanya fedha hizo. Hata hivyo, ni kweli kuwa walimu wa Wilaya ya Kusini

Unguja wamechangia fedha katika ujenzi wa Afisi ya Elimu ya Wilaya kwa ridhaa zao na kwa utaratibu waliokubaliana na Ofisi ya Elimu ya Wilaya yao bila ya kuishirikisha wizara. Hivyo, makusanyo hayo hayakusimamiwa na wizara na hakuna fedha iliyowasilishwa wizarani. Napenda ieleweke kuwa michango yote wanayochangishwa walimu ni ya hiari na walimu wanaelimishwa kwanza kabla ya kuchangia.

Baada ya maelezo hayo Mhe. Spika, naomba kumjibu kama hivi ifuatavyo:-

a) Fedha zilizokusanywa kutokana na michango ya hiari ya walimu kwa muda wa miaka mitano iliyopita kuanzia mwaka 2006 hadi mwaka 2010 ni Shs. 145,042,890/- hii ni sawa na milioni 28,000,000 kwa mwaka.

Fedha hizo haziwasilishi hazina kama ni mapato ya Serikali na ndio maana hazionekani katika bajeti ya wizara, kwa sababu ni michango ya hiari na si rahisi kukadiria kiwango cha fedha zitakazokusanywa na zinatumika kwa shughuli iliyokusudiwa mara tu baada ya makusanyo kukamilika, matumizi ya fedha hizo hufuata taratibu zilizowekwa na serikali, hufanyiwa ukaguzi na wakaguzi wa ndani na nje wa mahesabu ya serikali.

Kama nilivyotangulia kusema kuwa matumizi ya fedha hizo kuwa zinafuata kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za serikali na hesabu zake zinafanyia ukaguzi kama vile matumizi mengine ya wizara. Hivyo, si sahihi kudai kuwa maafisa waangamizi wa wizara wamekuwa wakizitumia fedha hizo bila ya kufuata utaratibu wa kanuni za matumizi ya fedha.

Wizara haina utaratibu wa kuwakata walimu fedha za michango katika mishahara yao, michango ya walimu hutoa kwa ridhaa zao na ndio maana baadhi ya walimu wachache hawachangii na hakuna hatua yoyote inayochukuliwa dhidi yao. Wizara inatenga fedha kwa ajili ya sherehe mbali mbali za kitaifa hata hivyo, fedha hizo ni chache mno na haziwezi kukidhi mahitaji ya sherehe zenyewe. Ahsante.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe sijui kama hii saa inakwenda sawa sawa, kwa mujibu wa saa ya pale juu muda umemalizika kwa saa yangu mimi bado dakika tano. Kwa hivyo, naomba niruhusu swali moja tu.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya mwisho kabisa na naomba nikupongeze sana kwa umahiri wako. Baada ya shukurani hizo Mhe. Spika, nina swali moja la nyongeza lenye kifungu a na b.

(a) Mhe. Naibu Waziri alipokuwa akijibu swali hili muhimu sana kwa maisha ya walimu Wazanzibari amekiri kwamba michango ya walimu ni michango ya hiyari kinyume kabisa na maelezo ya walimu na uoni wa wawakilishi wenyewe. Na kwa kuwa serikali imekiri kuwa michango hii ni ya hiyari. Je, kuanzia leo atakuwa tayari kutoa kauli hapa kwamba michango hii mwisho leo ili malalamiko ya walimu yaweze kumalizika.

(b) Kwa kuwa amesema fedha hizi zinakaguliwa nje na ndani ya wizara, na kwa kuwa hatujawahi kupokea ripoti ya *PAC* inayohusu ukaguzi wa mapato hayo. Je, anakusudia kutwambia kwamba *CAG* na *PAC* hawawajibiki?

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, kama nilivyotoa maelezo ya awali kwenye jibu mama kwamba michango hii ni kweli ya hiyari kwa walimu na ndio maana kuna walimu wachache hawachangii michango hii basi hatujawahi kumuadhibi mwalimu yeyote kutokana na kutokuchangia michango hii.

Kuhusu suala alilosema kwamba nitoe tamko hapa la kutaka walimu kutokuchangia michango hii naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba, kama nilivyoeleza kwenye jibu langu mama kuwa michango hii Mhe. Spika, inatusaidia sana katika sherehe zetu, sio katika sherehe za elimu tu. Kwa mfano, kama hii michango ambayo inasaidia uendeshaji wa vituo vya walimu hii ni michango ambayo wanatoa walimu na inawasaidia katika kuhakikisha kwamba wanajiendeleza siku hadi siku kitaaluma katika vituo hivyo. Sasa leo niseme kama hii isiwepo kweli tutaweza kuendeleza walimu hawa? Na itakuwa ni kwa faida ya nani?

Mimi nadhani Mhe. Spika, Wajumbe wa Baraza lako hili tukufu ni muhimu watusiadie, licha ya kwamba ni hiyari lakini kuwahamasisha walimu wetu umuhimu wa michango hii kwa sababu inawasaidia wao na sisi kwa upande wa sherehe zetu.

Lakini mbali ya hayo, kama hii michango ya Tamasha la Elimu Bila Malipo. Michango hii inatusaidia sana katika siku za sherehe hizi, inatoa motisha kwa walimu lakini pia kwa wanafunzi. Kwa mfano, pesa ambazo tunazipata hapa tunatoa zawadi kwa wanafunzi bora, kwa skuli bora, kwa hivyo, ni fedha ambazo zinazunguka na zinasaidia sana kuhamasisha walimu na wanafunzi wetu kuhakikisha kuwa elimu yetu inakwenda mbele.

Swali lake (b) alilouliza kama ambavyo nilizungumza awali kuwa fedha hizi hazionekani kwenye bajeti yetu kwa sababu haziendi Hazina. Lakini zinaonekana katika matumizi yetu ya wizara kwa sababu zinakaguliwa na wakaguzi wa ndani na nje. Vile vile si vibaya kama pesa hizi kwa bajeti inayokuja tukaziweka katika bajeti yetu na kueleza kuwa kwa mwaka huu tumekusanya kiasi fulani kwa ajili ya matumizi fulani. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Waheshimiwa Wajumbe naomba mniwie radhi kuna salamu mbili za rambirambi za wenzetu wa karibu sana katika shughuli zetu za Baraza ambazo nazo tulizipokea, bahati mbaya tuliweka pahala ambapo barua hiyo sikuweza kuiona mara moja. Kwa hivyo, naomba nichukue nafasi hii pia kupitia kwangu kukupeni salamu za rambirambi kutokana na misiba iliyotufika iliyotoka kwa ndugu yetu Dr. William F. Shija, *Secretary-General* wa *CPA*. Barua inasomeka kama ifuatavyo:-

Rt Hon. Pandu Ameir Kificho, MHR
Speaker of the House of Representatives,
House of Representatives,
P.O Box 902,
Zanzibar,
Tanzania.

Dear Hon. Speaker,

On behalf of the Hon. Chamal Rajapaksa, MP, Speaker of Parliament of Sri Lanka, and President of the Association, The Rt Hon. Sir Alan Haselhurst, MP. Chairperson of the CPA International Executive Committee. Hon. Dr Nafisa Shah, MNA, Parliament of Pakistan and Vice Chairperson of the CPA Executive Committee, Hon. Marwick Khumalo, MP, Parliament of Swaziland. Treasurer of the Association, and Hon. Alix Boyd-Knights, MP Speaker of the Legislative Assembly, Republic of Dominica, and CWP Chairperson, Members of the Executive Committee, and on my own behalf, I wish to express my deepest sorrow and sadness at the loss of and property due to the recent tragic incident of the sunken boat in Zanzibar, causing untold grief to many families in your beautiful and peaceful country.

The Commonwealth Parliamentary Association joins the Parliament and the people of Zanzibar in mourning the loss of the destruction caused to that effect.

May the souls of the deceased Rest in Eternal Peace.

With kindest regards and wishing your country quick recovery.

Your Sincerely,

Dr. William F. Shija
Secretary-General

Hizo ni salamu kutoka kwa ndugu yetu Dr. Shija Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Mabunge, Jumuiya ya Madola. Naomba salamu hizo pia Waheshimiwa Wajumbe tuzipokee.

Salamu nyengine za rambirambi ni salamu zilizotoka kwa wenzetu wa *Arusha Wazee Sport Club*, nazo zinasomeka kama ifuatavyo:-

CONDOLENCE MESSAGE TO BARAZA LA WAWAKILISHI
AND BY EXTENSION TO THE PEOPLE OF ZANZIBAR

Today is sad, very sad day in Zanzibar, Tanzania, East Africa and the entire African continent because we are ONE human family. America will always remember 9/11. As from today Tanzania will remember 9/10.

As part of a time-honored relationship between Baraza la Wawakilishi where every year MPs and staff travel for sportsevents in Easter and September respectively. AWC and happy guests were planning the third day of their visit, featuring a trip to the Tarangire National Park, when joy brutally turned into sadness with news of the capsizing of MV Spice Islanders as it sailed from Unguja to Pemba.

*We did all to facilitate our guests led by the charismatic and very friendly **Speaker Pandu Ameir Kificho** and 7 Ministers and MPS and staff to travel back to Zanzibar but we could not leave it at that. Too many lives were lost, too many careers were broken, too many dreams were ruined. At our Club meeting yesterday, it was unanimously decided that a delegation travels to Zanzibar to express our heartfelt sympathy on this tragic occasion. In the same way the Americans have transformed the tragedy of losing nearly 3000 people in a day into a strong determination to fight evil and build unity, so also the Zanzibaris must use the loss of 300 people in one day to fight neglect and incompetence.*

Zanzibar must come out a stronger, better and greater country after 9/10! Like Tony Blair said, you must also say: "I can only go one way. I've not got a reverse gear". Go forward people of Zanzibar life must continue. That is our message to you all.

On behalf of Wazee Arusha in particular and the loving people of Arusha District who all supported our years partnership, we hereby extend heartfelt condolences to the Baraza la Wawakilishi and the people of Zanzibar.
*Again, we strongly commend government's efforts so far, to rescue hundreds of women and children even by night, and the creation of the **Help Zanzibar Fund** by a token gift of 1.500 000 TSH. You have proved your commitment to the sanctity of human life. Our pockets are small but our hearts with you are big and heavy. Money will never replace life but may every shilling help a child mother or father to face lice, even after 9/10/*

God bless the people of Zanzibar.
God bless the people of Tanzania.

Thank You.
On behalf of Arusha Wazee Sports Club
Aatsa Atogho, Deputy Chairperson,
Ally Mamuya, Secretary General
Stella Klemanna, Club Member,
Zanzibar, 13th September, 2011.

Waheshimiwa Wajumbe hizi ni salamu ambazo pia naomba mzipokee zimetoka kwa wenzetu wanamichezo *Arusha Wazee Club*. Nakushukuruni ahsanteni.

KAULI ZA MAWAZIRI

Ripoti tatu (3) za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2009/2010

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa na afya njema na kutelekeza majukumu yetu kwa lengo la kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, pili kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Tumbatu na kwa niaba ya watumishi wenzangu wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora niendelee

kuungana na Wazanzibari wote katika kutoa mkono wa pole kwa familia ambazo zimepoteza ndugu zao kwa ajili ya meli na Mwenyezi Mungu awape makazi mema peponi AMIN.

Mhe. Spika, shukurani zangu kwako wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuwasilisha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, shukurani za pekee nazitoa kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Ali Mohammed Shein kwa busara na hekima kubwa aliyonayo na anayoitumia kwa hatua ya kuniagiza kuwasilisha Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali mara tu baada ya kuipokea ripoti hiyo.

Mhe. Spika, Wajumbe wako watakumbuka kuwa si muda mrefu uliyopita niliwasilisha ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2008/2009, na hii leo tayari nawasilisha ripoti hii ya mwaka 2009/2010. Hii ni ishara tosha kwamba Dr. Ali Mohammed Shein ni Muumin mkubwa wa utawala bora.

Naomba kuchukua nafasi hii kuwasilisha ripoti tatu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2009/2010 ambazo zimejumuisha ripoti ya ukaguzi wa mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2010. nchi iliyokaguliwa pamoja na Ripoti ya Udhibiti na Utunzaji wa Rasilimali za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Spika, ripoti hizi zinawasilisha kwa kufuata muongozo wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu 112(5), ambapo kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu anawajibika kuwasilisha ripoti hizo.

Kitendo cha uwasilishaji wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa kila mwaka inaashiria kuwepo kwa uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za umma na kuhakikisha kwamba kunakuwa na utawala bora katika utunzaji wa rasiliamli hizo. Ripoti hizi zimeeleza hali halisi ya uwekaji wa mahesabu ya kiserikali pamoja na udhibiri na utunzaji wa mali za umma ikizingatiwa kupatikana kwa tija kwa kila rasilimali ya umma inayotumika kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar, ikiwemo uhalisia wa tija iliyopatikana katika matumizi ya rasilimali za umma pamoja na fedha zinazotolewa na wahisani wa maendeleo. Aidha, kwa njia ya misaada au mikopo kwa kufanikisha miradi ya maendeleo ya wananchi kwa ujumla.

Lengo kuu la ripoti hizi ni kupata ufanisi katika matumizi ya fedha, utunzaji wa rasilimali pamoja na uendeshaji wa shughuli za serikali kwa kuzingatia kwamba fedha zinatumika kwa mujibu wa sheria na taratibu za fedha ziliopo na kuhakikisha kwamba sheria na taratibu hizo zinafuatwa ipasavyo.

Mhe. Spika, majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa mujibu wa katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 kifungu cha 112, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anawajibika kuidhinisha fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kufanya ukaguzi wa mahesabu na kutoa ripoti juu ya ukaguzi huo.

Upeo na Madhumuni ya Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2009/2010.

Ripoti hizi zimekusanya taarifa za ukaguzi wa mahesabu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na mashirika yake. Kwa upande wa ripoti ya mahesabu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inajumuisha taarifa ya mapato na matumizi ya fedha kutoka Mfuko wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kama ilivyoidhinishwa kwa mujibu wa sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi kwa kipindi cha mwaka 2009/2010.

Aidha, kwa upande wa ukaguzi yakinifu ripoti inaelezea ukaguzi uliofanywa katika miradi ya maendeleo ya wananchi iliyokaguliwa pamoja na udhibiti na utunzaji wa rasilimali za umma. Kwa vile ofisi imeanza kufanya ukaguzi yakinifu, tumelazimika kuchagua maeneo machache kwa kutumia rasilimali ziliyopo. Kutokana na hilo, ukaguzi yakinifu uliofanywa ulichagua maeneo maalum ambayo taarifa ya ukaguzi wake ndizo zilizoripotiwa. Ukaguzi huo umefanywa kwa kufuata kanuni, sheria na taratibu za ukaguzi ziliopo kwa kuzingatia viwango vya ukaguzi vilivyowekwa kitaifa na kimataifa.

Kiwango cha uwekaji wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, kiwango cha uwekaji wa Hesabu za Serikali kimeimarika na kwa kiasi kikubwa kimechangiwa na kuwepo mfumo mzuri wa udhibiti na utumiaji wa fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali. Kuwepo kwa utaratibu wa malipo kupitia mfumo wa mtandao wa *IFIMS* kumesaidia kuleta maendeleo makubwa katika utunzaji na uwekaji wa hesabu katika taasisi za serikali.

Vile vile hatua hiyo ya maendeleo inatokana na kuwepo mfumo mzuri wa uwekaji wa kumbukumbu za mapato na matumizi ya fedha za serikali. Kutokana na hilo kumepelekea kuwepo kwa udhibiti mzuri wa fedha na mali za serikali pamoja na uwajibikaji wake.

Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inaendelea kutoa ushauri na miongozo kwa taasisi mbali mbali za serikali juu ya kuimarisha viwango vya uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu ikiwemo madaftari mbali mbali ya hesabu pamoja na uhifadhi na udhibiti wa vifaa na mali za serikali.

Afisi inashauri viongozi na watendaji wakuu wa serikali kufuatilia mwenendo mzima wa fedha kuanzia ukusanyaji wa mapato na matumizi, pamoja na uhifadhi na udhibiti wa rasilimali za umma katika taasisi wanazozisimamia na kusimamia utekelezaji wa sheria zilizopo. Kufanya hivyo kutaongeza ufahamu na ufanisi utakaosaidia kupunguza kwa kiasi kikubwa dosari za kiutendaji zinazojitokeza mara kwa mara kuelekea katika utawala bora, kwenye mapato na matumizi ya fedha na mali za umma.

Mhe. Spika, kuimarika kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali inaendelea kuimarisha huduma za ukaguzi zinazotolewa kwa taasisi mbali mbali za serikali pamoja na baadhi ya miradi ya maendeleo. Aidha, inaendelea kuliwekea kipaumbele suala la mafunzo kwa wafanyakazi na kuhakikisha inawasomesha wafanyakazi wengi mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi katika vyuo mbali mbali nchini na nje ya nchi na hasa katika fani mpya za ukaguzi.

Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 afisi imeweza kukamilisha muongozo wa ukaguzi na kuanza kutumika muongozo huo ambao unakwenda sambamba na miongozo ya ukaguzi inayokubalika na Jumuiya za Ukaguzi Duniani.

Katika kipindi cha mwaka 2009/2010 afisi imeanza kufanya mabadiliko katika ukaguzi na kuelekea katika ukaguzi yakinifu pamoja na ukaguzi wa mazingira kwa lengo la kuona ufanisi wa udhibiti na matumizi ya rasilimali za umma. Vile vile kwa upande wa mahesabu ya mwaka 2010/2011 ukaguzi wake umeshaanza na unaendelea vizuri kwa baadhi ya taasisi za serikali pamoja na mashirika ya umma, tunatarajia kuendelea na kazi za ukaguzi kwa taasisi nyengine za serikali ikiwemo miradi ya maendeleo ya wananchi na kutoa taarifa ya ripoti hizo kwa mujibu wa sheria ziliyopo.

Mambo yaliyobainika katika ukaguzi kwa mwaka 2009/2010.

Kwa mwaka 2009/2010 kumekuwa na mafanikio makubwa katika uwekaji wa kumbukumbu za mahesabu katika taasisi mbali mbali za serikali. Hata hivyo, kumejitokeza dosari ndogo ndogo za kiutendaji ambapo hoja mbali mbali za ukaguzi zilizotolewa kuhusiana na dosari hizo zilipatiwa ufumbuzi kwa kurekebishwa baadhi ya kasoro hizo na kutolewa ufafanuzi pamoja na maelezo yaliyokosekana wakati wa ukaguzi.

Aidha, upande wa ukaguzi yakinifu uliofanywa imebainika kwamba miradi mingi haikuweza kufanikisha lengo lililokusudiwa kwa vile huduma zilizotegemewa hazikuweza kupatikana kwa wananchi na kupelekea kutokupatikana kwa tija na ufanisi wa miradi hiyo.

Ukusanyaji wa mapato ya kawaida

Kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 kumekuwa na ukusanyaji mzuri wa mapato na kukusanya jumla ya TShs. 213.96 bilioni ikiwa ni ongezeko la TShs. bilioni 1 la makadirio zilizokusanywa. TShs. 212.99 bilioni kwa mwaka huo. Aidha, imeonekana bado jitihada za makusudi zinahitaji kuchukuliwa katika kuimarisha vianzio mbali mbali vya mapato ya ndani ya nchi.

Matumizi ya Kazi za Kawaida

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 hali ya mgawanyo wa fedha kwa matumizi yameonesha kuwepo na mafanikio makubwa katika mgawanyo wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida, kwa mujibu wa taarifa za matumizi ya kawaida kwa mwaka 2009/2010 yalifikia asilimia 95.07 ya makadirio.

Matumizi ya Maendeleo

Mhe. Spika, kwa mwaka 2009/2010 serikali ilijipangia kutumia kiasi cha TShs. 239.9 bilioni kwa matumizi ya kazi za maendeleo. Kati ya hizo TShs. 40.7 bilioni ilikuwa ni mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na TShs. 199.2 bilioni ilikuwa ni misaada na mikopo kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Ukaguzi umebaini kwamba matumizi halisi yaliyofanyika katika kipindi hicho yalikuwa ni TShs.109.3 bilioni ambapo mchango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ulikuwa ni TShs. 40.03 bilioni ambapo ni sawa na asilimia 98.4 ya makadirio. Kwa upande wa fedha kutoka kwa wahisani wa maendeleo ilikuwa ni TShs. 69.26 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 34.8 za makadirio.

Miradi ya Maendeleo ya Wananchi

Mhe. Spika, miradi ya maendeleo ya wananchi ni miradi inayofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kutoka katika mfuko mkuu wa hazina ya Serikali ya Mapinzi ya Zanzibar, kupitia Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ambayo ndio inayosimamia upatikanaji wa fedha za miradi hiyo. Miradi mingi ya wananchi inalenga kuimarisha huduma mbali mbali za jamii, ikiwemo afya, elimu, maji safi na salama na kadhalika. Miradi hiyo ilikuwa ni ya ujenzi wa maskuli, vituo vya afya, visima vya maji na kadhalika.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kwa miradi iliyokaguliwa, fedha zilizotumika kwa mikoa ni kama ifuatavyo.
Mkoa wa Kusini Unguja Shs. 20 milioni, Mkoa wa Kaskazini Unguja Shs. 20.5 milioni, Mkoa wa Mjini Magharibi Shs. 20 milioni, Mkoa wa Kaskazini Pemba Shs. 15.8 milioni na Mkoa wa Kusini Pemba Shs. 11 milioni.

Miradi ya maendeleo ya *TASAF*

Mhe. Spika, miradi ya maendeleo ya TASAF ni miradi ya wananchi inayopata michango ya fedha kutoka Benki ya Dunia pamoja na nguvu za wananchi wa maeneo husika ambapo usimamizi wa upatikanaji wa fedha za miradi hiyo upo chini ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Miradi mingi ya wananchi inalenga kuimarisha huduma mbali mbali za jamii, ikiwemo afya, elimu, maji safi na salama, barabara, kilimo na ufugaji na kadhalika.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopatikana kwa miradi iliyokaguliwa, fedha zilizotumika kwa kila mkoa ni kama ifuatavyo.

Mkoa wa Mjini Magharibi Shs. 213.28 milioni, Mkoa wa Kusini Unguja Shs. 277.7 milioni, Mkoa wa Kaskazini Shs. 285.4 milioni.

Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Serikali

Mhe. Spika, kwa upande wa Udhibiti na Utunzaji wa Mali za Serikali ukaguzi uliofanyika imebainika kwamba rasilimali nyingi zinazomilikiwa na taasisi mbali mbali za serikali hakuna udhibiti na utunzaji mzuri wa mali hizo.

Aidha, imebainika kwamba taratibu na miongozo kwa mujibu wa sheria ya fedha na sheria ya manunuzi hazifuatwi ipasavyo. Mali nyingi zimekutwa zikiwa katika hali mbaya ambapo baadhi yake zilikuwa zinahitaji matengenezo madogo ili ziweze kutumika kwa ajili ya shughuli za taasisi hizo. Baada ya ukaguzi imebainika kwamba mali hizo zingeweza kutumika baada ya

kufanyiwa marekebisho au matengenezo madogo. Hali hii inasababisha hasara kubwa kwa serikali kwa vile inaendelea kugharimia huduma zinazotolewa katika kuhifadhi mali hizo.

Aidha, ukaguzi umebaini kwamba wizara na taasisi nyingi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haziandai mpango wa manunuzi ya mwaka kwa mahitaji ya vifaa na huduma mbali mbali zitakazo hitajika kwa matumizi ya wizara na taasisi hizo. Kama inavyoelekeza sheria nambari 9 ya manunuzi ya mwaka 2005 kifungu nambari 19.

Kutokuwa na mpango wa manunuzi kunapelekea kuongezeka gharama za manunuzi na kununuliwa bidhaa katika wakati usiohitajika. Ukaguzi umebaini kwamba wizara na taasisi nyingi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haziweki daftari za kuhifadhi mali za kudumu yaani *fixed assert register* kwa mujibu wa kifungu nambari 264 cha kanunuzi za fedha za Zanzibar ya mwaka 2005, kila taasisi ya serikali inawajibika kuweka daftari la kumbukumbu za mali zote zinazomilikiwa na taasisi husika ambapo katika daftari hilo hupaswa kuingizwa mali zote zinazomilikiwa na taasisi hizo.

Kutokuwa na daftari hilo kunaweza kusababisha kutokujua idadi na thamani ya mali zinazomilikiwa na taasisi husika na kupelekea upotevu wa mali hizo na kusababisha hasara kwa taasisi na serikali kwa ujumla. Ukaguzi umebaini kwamba wizara na taasisi nyingi zinamiliki majengo mbali mbali lakini hazina hati miliki za majengo hayo. Kutokuwepo kwa hati miliki za mali hizo kunasababisha kutokuwepo na uhalali wa umiliki wa mali hizo.

Changamoto Ziliopo

Mhe. Spika, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inakabiliwa na changamoto mbali mbali za kiutendaji ambapo zinahitajika kutafutiwa ufumbuzi wa haraka mara changamoto hizo zinapojitokeza.

Changamoto zinazotukabili zinatokana na mabadiliko katika kazi za ukaguzi pamoja na mabadiliko ya mara kwa mara katika mifumo ya fedha pamoja na viwango vya uwekaji wa kumbukumbu za hesabu na ufungaji wa mahesabu ya mwisho wa mwaka kunasababisha athari katika utendaji wa shughuli za uhasibu na ukaguzi.

Malango ya Baadae

Mhe. Spika, afisi imeshatayarisha mpango wa mkakati yaani *strategic plan* mpya kwa miaka mitatu, kuanzia mwaka 2011 hadi 2014. Mpango wa mkakati huo umejikita katika maeneo ya kuimarisha afisi kiutendaji, pamoja na kuongeza idadi ya wafanyakazi wenye taaluma mbali mbali zitakazo saidia kuimarisha kazi za ukaguzi. Mpango wa mkakati huo umekusudia kuendeleza jitihada zitakazochukuliwa wakati wa kutekeleza mpango wa mkakati uliopita wa miaka mitatu kuanzia mwaka 2007 hadi 2011 ambapo utekelezaji wake umeleta mafanikio makubwa ya kiutendaji katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Katika Mpango wa Mkakati huo mpya, afisi imekusudia kutekeleza malengo yafuatayo.

1. Kuimarisha uwezo wa Afisi ya Mdhaibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesababu za Serikali.
2. Kushajihisha usimamizi uwajibikaji wa masuala ya fedha na mali za umma.
3. Kushirikiana na kuimarisha uwezo wa kuitendaji kwa taasisi zinazosimamia uwajibikaji pamoja na kuimarisha mawasiliano na wadau wetu.

Hitimisho

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena natoa shukrani zangu kwako na kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kushirikiana na mimi katika kutekeleza majukumu ya wizara yangu.

Vile vile naomba niwashukuru kwa dhati wajumbe wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi, inayoongozwa na Mwenyekiti wake Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Chake Chake, Mhe. Omar Ali Shehe. *(Makofi)*.

Mhe. Spika, ni imani yangu kwamba wataifanyia kazi ripoti hii hasa baada ya kupokelewa rasmi na Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa uwasilishaji wa ripoti hiyo. Kabla Waheshimiwa Wajumbe hatujaendelea, niwaombe wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Aifisi za Viongozi Wakuu washirikiane na Mwenyekiti ili kwenda kujadili ripoti ambayo inategemewa iwasilishwe kesho kutoka Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Kwa hivyo wanatakiwa na wao kama kamati watowe maoni yao juu ya ripoti hiyo, kwa hivyo watakuwa na mkutano wa kamati hivi punde na Mwenyekiti anawaomba mukutane ili kujadili taarifa hiyo, ahsante.

Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika.

Hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika (PAC) Juu ya Uwasilishaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Zanzibar kwa Kipindi cha Mwaka 2009/2010.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika(PAC): (Mhe. Omar Ali Shehe): Mhe. Spika, awali ya yote naomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mtukufu, kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu kwa nia ya kuwatumikia wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kabla sijaeleza yahusianayo na ripoti kwa niaba ya Kamati yangu ya PAC naomba kutoa pole kwa familia ya marehemu Mhe. Mussa Khamis Silima na wananchi wote wa Jimbo la Uzini na wale wote waliopatwa na maafa, kufuatia janga kubwa la kuzama kwa meli ya Mv. Spice Islender iliyotokea usiku wa kuamkia Jumamosi ya tarehe 10/9/2011 katika mkondo wa Nungwi Wilaya ya Kaskazini A Unguja. Tunamuomba Mwenyezi Mungu aziweke mahala pema

peponi roho za marehemu wote waliofariki katika ajali hiyo, pia tunamuomba Mwenyezi Mungu awape nafuu na moyo wa subra wale wote waliopoteza ndugu, jamaa na marafiki kadhalika waliopata athari za kisaikolojia na waliopotelewa na mali zao.

Mhe. Spika, kwa kuwa inasadikiwa kwamba uzembe wa kiutendaji ni moja ya sababu zilizopelekea kutokea kwa ajali hiyo, tunaitaka Serikali kwa mara nyengine tena kuchukua hatua madhubuti za kunusuru maisha ya watu na mali zao katika suala zima la usafiri ndani na nje ya visiwa vyetu. Kwa hili kubwa lililotokea na ambalo hadi sasa machozi hayajakauka katika nyuso za Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla, tunaomba kwa Tume iliyoundwa na Mhe, Rais kwamba pamoja na mapungufu yake ambayo yanaendelea kulalamikiwa na wananchi, tunaiomba ifanye kazi kwa uhuru na uwazi na kwamba wale wote watakaobainika kwa namna moja ama nyengine kuhusika na kutokea kwa msiba huo, wachukuliwe hatua zitakazoonekana na kila mmoja wetu kama ni moja ya mkakati wa kukomesha uzembe katika uwajibikaji katika sekta ya Umma na sekta binafsi.

Mhe. Spika, naomba sasa nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako Mhe. Spika kwa kunipa fursa hii ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kuzungumza machache na ya muhimu yahusianayo na uwasilishaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mwaka 2009/2010. Ripoti zilizowasilishwa na Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora hivi punde ni ripoti inayohusu ukaguzi ya mwaka 2009/2010, ripoti ya Ukaguzi yakinifu ya Miradi ya Maendeleo ya Wananchi ya mwaka 2009/2010 pamoja na ripoti ya Ukaguzi yakinifu ya mali za Umma ya mwaka 2009/2010.

Mhe. Spika, hatua hii ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya kuwasilisha ripoti tatu (3) kwa pamoja ni hatua ya kihistoria kwa maendeleo ya Baraza, Utawala bora nchini pamoja na maendeleo ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali. Hii ni mara ya kwanza kwa Ofisi ya Mdhibiti kuandaa na kukamilisha ripoti zihusianazo na Ukaguzi yakinifu yaani *Value for Money Auditing* badala ya kaguzi tulizozizowea za uhalali wa matumizi ya fedha za umma yaani *Public Financial Auditing*. Kwa hatua hii napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kupitia kwako Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi kubwa na nzuri iliyopelekea ripoti hizo leo hii kukabidhiwa Baraza hili kwa niaba ya wananchi.

Mhe. Spika, hatua hii inadhihirisha utashi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga na kuimarisha misingi ya utawala bora katika eneo la matumizi sahihi na yenye tija ya fedha za umma. Kadhalika inadhihirisha utashi wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wa kwenda sambamba na mabadiliko ya kiukaguzi wa Kimataifa. Ingawa Mdhibiti kaamua, kathubutu na hatimae leo hii ameweza kuwasilisha ripoti hizo, naamini na ndivyo ilivyo kwamba ufanikishaji na ukamilifu wa ripoti hizo haukuwa wala hautokuwa rahisi kutokana na changamoto mbali mbali zinazohusu kufanikisha aina hii ya ukaguzi ambayo ina faida kubwa kwa maendeleo ya taifa letu.

Mhe. Spika, kamati inaiomba sana Serikali ifanye kila aina ya juhudi kuiwezesha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili iweze kumudu kuajiri wataalamu wake wenye fani mbali mbali ambao wataiwezesha Ofisi hiyo muhimu kuweza kufanya ukaguzi yakinifu, ukaguzi kupitia mitandao ya komputa na ukaguzi wa kimazingira. Kwani huko ndiko

wajanja walikojichimbia baada ya hatua nzuri na mafanikiao yatokanayo na kazi ya ukaguzi iliyofanywa na Mkaguzi tangu kuanzishwa kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi na tangu kuazishwa kwa Kamati ya PAC.

Sambamba na hilo, tunaiomba serikali iifanye aina hii ya ukaguzi iwe ni endelevu kwa kuangalia upya maslahi ya watumishi na wakaguzi katika Ofisi hii Ili kuwaepusha na udokozi au kurubuniwa kwa rushwa, inawezekanaje wafanyakazi wa taasisi zinazoshughulikia fedha wakajengewa mazingira mazuri ya "kuridhika" na wanachokipata, lakini watendaji hawa wenye jukumu zito la kuwakagua wenye fedha wao wakawa na mazingira duni?. Nadhani ni katika mazingira haya ndiyo yanayoweza kupelekea zoezi la ukaguzi likawa gumu na tusiweze kufikia lengo tulilokusudia. Kawaida mwenye pesa hukaguliwa na mwenye pesa na kamwe mwenye pesa hakaguliwi na mtu mwenye njaa.

Mhe. Spika, baada ya ripoti hizi kuwasilishwa kwenye Baraza lako tukufu leo hii, kinachofuata sasa ni ripoti hizi kukabidhiwa kwa Kamati yako ya PAC kwa ajili ya kuzifanyia kazi kwa mujibu wa matakwa ya Kanuni za Baraza kifungu cha 115 na kanuni za fedha ya mwaka 2005, ambapo kukabidhiwa kwa ripoti hizi kwa Baraza letu, sasa kuna haulisha changamoto zinazoikabili Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu katika utekelezaji wa majukumu ya ukaguzi yakinifu hadi kuhamia kwenye kamati ya PAC katika ufuatiliaji wa ripoti hizo na mambo mengine yanayohusu kazi za PAC kwa mujibu wa Kanuni.

Mhe. Spika, changamoto kubwa inayoikabili Kamati ni uwezo mdogo wa Kamati wa kuifanyia kazi ripoti hizi zenye aina mpya ya ukaguzi, kwa vile eneo hili la ukaguzi linahitaji utaalamu. Kamati inaomba kupatiwa mafunzo kabla ya kuanza kufanyika kazi mwezi Disemba mwaka huu Inshaallah.

Changamoto nyengine inayoikabili Kamati, kufuatia kukabidhiwa ripoti hizi ni tatizo la muda la ufanyaji kazi wa Kamati. Hapa naomba ikumbukwe kuwa kuwasilishwa kwa ripoti hizi tatu zinalifanya Baraza na Kamati kuwa na ripoti nne mkononi ambazo hazijafanyiwa kazi na ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi na kutolewa ripoti zao katika muda uliopangwa.

Mhe. Spika, kwa siku 20 tu za kazi tulizobakia nazo mwaka huu kabla hatujawasilisha ripoti yetu katika kikao cha March/ April-2012, yaani siku 10 za kazi kwa Kamati mwezi wa December na siku 10 za kazi mwezi wa March, hazitoshi kuifanya Kamati iifanyie uchunguzi wa ndani Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ya mwaka 2008/2009 ile tuliyonayo mikononi na ambayo bado tunaendelea nayo, ingawaje utendaji huo hukidhi haja tu ya kutuwezesha kutoa taarifa ya yale mambo ya msingi yaliyoripotiwa kwenye ripoti hiyo.

Lakini iwapo tungetaka kukidhi utashi wa maelekezo na makusudio ya Kanuni zetu, yaani kwa namna Kamati inavyoona inafaa tuchunguze hesabu zote za serikali na asasi zake au tuchunguze kwa undani fedha zilizooneshwa katika Makadirio ya Matumizi ya Serikali na Mashirika yake kwamba zimetumika kama zilivyokubaliwa na Baraza ama kujiridhisha kwamba matumizi ya fedha za Umma yamefanywa chini ya Mamlaka inayohusika na kwamba matumizi hayo yamezingatia thamani halisi ya fedha kama kifungu cha 115 (2) (c) na (3) cha Kanuni za Baraza zinavyoelekeza.

Mhe. Spika, kwa kufanya hivyo, basi tungehitaji zaidi ya wiki 8 tunazopewa kila mwaka, hivyo, ni sawa na kusema katika majukumu matano ya Kanuni za Baraza, mpaka leo Kamati ya P.A.C inatekeleza jukumu moja tu la kuchunguza ripoti za Mdhibiti tena kijuu juu kutokana na muda kuwa mdogo. Katika hili Kamati inaendelea kusisitiza haja ya kuongezewa muda wake wa kazi angalau kwa kuanzia tupate wiki 3 kwa kila muhula wa kazi.

Mhe. Spika, sambamba na changamoto hiyo, Leo tumeshakabidhiwa ripoti 3 kwa pamoja na zote zinatakiwa zifanyiwe kazi mara moja na kwa ufanisi mkubwa, bila ya shaka muda wa kazi za Kamati nao ni lazima uongezwe, vyenginevyo kutakuwa na mrundikano wa kazi za ripoti hizo za Mdhibiti kwa Baraza letu na kwa Kamati ya P.A.C.

Naomba ifahamike wazi kwamba, juhudi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutoa ripoti kwa wakati hadi ya mwaka 2009/2010 na sasa anajiandaa kutoa ripoti nyengine mpya za mwaka 2010/2011 hapo mwakani, zinapaswa kuonekana kuwa ni changamoto ambayo inahitaji kupatiwa ufumbuzi ikiwa ni pamoja na kutengwa muda wa ziada kwa Kamati ya P.A.C ili kuzifanyia kazi ripoti hizo kabla ya kuachwa nyuma na kasi ya Mdhibiti na hivyo kuepukana na mrundikano wa kazi yaani *Back log* kama ilivyotokea mwaka 2008 wakati ilipokabidhiwa na kulazimika kuzimaliza ripoti 3 za 2004/2005; 2005/2006 na 2006/2007 kwa pamoja na kuzitolea ripoti zake ndani ya mwaka mmoja. Hali kama hii husababisha mzigo mkubwa kwa Baraza kutokana na ufinyu wa Bajeti yake ya kazi za Kamati, hali iliyopelekea kila Kamati kupatiwa wiki 8 tu ya kazi ndani ya mwaka mzima. Hali ambayo kwa namna yoyote huzifanya Kamati zetu za Kudumu za Baraza zifanye kazi kwa kuripua, kitu ambacho kitaleta hasara kubwa kwa wananchi na taifa.

Mhe. Spika, katika utekelezaji ama utatuzi wa changamoto hizi kwa Baraza na kamati ya P.A.C, naiomba sana Wizara ambazo ni wadau wa masuala haya kama vile Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo pamoja na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais zitusaidie kutatua changamoto hizi zinazolikabili Baraza na Kamati ya *P.A.C* kwa sasa.

Mhe. Spika, naomba niitumie fursa hii kuikumbusha serikali kwa mara nyengine tena kuzifanyia kazi na kuzichukulia hatua za wazi wazi ripoti za Kamati ya *P.A.C* baada ya kuzifanyia kazi ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwani Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu pamoja na Kamati ya *P.A.C* zimeanzishwa na zinatekeleza majukumu yao kwa mujibu wa Katiba, Sheria na Kanuni zetu. Kitendo cha kuzidharau na kutokuzifanyia kazi ripoti zote 2 katika uwazi yaani *transparency* na kuwawajibisha waliohusika na ubadhirifu wa matumizi mabaya ya fedha za Umma, ama Serikali yenyewe inaposhindwa kuwajibika ipasavyo kutokana na taarifa za ripoti hizi, kutawafanya wananchi wetu nao wapoteze imani yao kwetu kama Baraza na Serikali yao na matokeo yake thamani halisi ya fedha zinazotumika kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pamoja na kamati zetu zitapaswa nazo zichunguzwe ili wananchi wafahamu uhalali wa matumizi yake. Hiyo ndio maana ya *Value for money.* Ili kuepusha hali hiyo isitokee tunaitaka serikali kuzifanyia kazi ripoti hizi kwa ukamilifu wake na mapendekezo ya kamati ya Baraza hili, msisitizo katika hili ukiwekwa kwa kamati ya *P.A.C.*

Mhe. Spika, naomba nimalizie maelezo yangu kwa niaba ya Kamati kwa kumpongeza kwa mara nyengine tena, Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mashirikiano makubwa wanayotupa kwenye Kamati yetu ambayo yanatuwezesha kutekeleza vizuri majukumu yetu tuliyopewa na taifa pamoja na wananchi wetu.

Naomba nimshukuru sana Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa mashirikiano na mashauriano ya mara kwa mara, kati ya Afisi yake, Makatibu wa Kamati pamoja na Kamati yetu kwa ujumla, Kamati ambayo imekuwa na mashirikiano makubwa yanayotuwezesha kufanikisha majukumu yetu kwa ufanisi mkubwa. Naomba kuwapongeza kwa dhati Wajumbe wa Kamati yangu ya *P.A.C* na kuwaomba wazidishe mashirikiano miongoni mwao.

Wajumbe wa Kamati ni hawa wafuatao:

1. Mhe. Omar Ali Shehe	Mwenyekiti
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Mjumbe
4. Mhe. Farida Amour Mohammed	Mjumbe
5. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Mjumbe
6. Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Mjumbe
7. Mhe. Shadya Moh'd Suleiman	Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Mjumbe
9. Ndg. Abdalla Ali Shauri	Katibu
10. Ndg. Othman Ali Haji	Katibu

Mhe. Spika, naomba nikushukuru mara nyengine tena kwa kunipa nafasi hii pamoja na kunivumilia kuutumia muda wako adhimu katika kuiwasilisha maoni ya Kamati juu ya uwasilishwaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2009/2010. Ni matumaini yangu na ya Kamati kuwa mapendekezo ya Kamati yamesikika na yatafanyiwa kazi kama tulivyoshauri.

Mwisho nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza, kwa ustahamilivu na usikivu wenu kwa kipindi chote nilichowasilisha maoni ya Kamati. Ni imani yangu kuwa mtaunga mkono mapendekezo ya Kamati kwa manufaa na maslahi ya Wananchi na Baraza lao la kutunga Sheria.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, ripoti imewasilishwa pamoja na taarifa ya Kamati ya *PAC* pia imewasilishwa. Shughuli yote hiyo nzima ambayo imesifiwa na pande zote mbili, inafanyika wakati Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yupo hapa pamoja na timu yake, basi ninawaomba wasimame. Nawashukuru, ahsante sana kwa kuja kusikiliza kazi yenu ambayo mumetuletea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, ripoti hii kama kawaida ipo chini ya utaratibu wa Kauli za Serikali, ambapo haitajadiliwa isipokuwa kama kuna maswali tuulize, ili hatimaye tuipokee rasmi na kuikabidhi kamati inayohusika kwa ajili ya kuifanyiakazi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nataka nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali machache kuhusiana na ripoti hii. Lakini kabla ya hapo naomba uniruhusu kuungana na wenzangu kutoa pole kwanza kwa msiba wa ndugu yetu mpendwa, mwenzetu marehemu Mhe. Mussa Khamis Silima kwa kifo chake ambacho kilichotokezea.

Kwa hivyo, tunaiomba familia ya marehemu iwe na busira kutokana na msiba huu mzito. Kilichobakia ni kwamba tunamuomba Mwenyezi Mungu amsamehe makosa yake marehemu, amuondoshee adhabu ya kaburi na ampe makaazi yaliyomema peponi Amin.

Mhe. Spika, vile vile niwape pole ndugu zetu wote waliopata msiba mkubwa, ambao katika meli iliyozama ya *Spice Islander I*. Kwa hivyo, tunamuomba Mwenyezi Mungu awape makaazi yaliyomema peponi, pia na familia tunaomuomba Mwenyezi Mungu awape subira na awape nguvu nyengine wale waliopotelewa na ndugu zao, ili waweze kuendesha maisha yao kwa salama.

Mhe. Spika, baada ya hayo sasa nataka niipongeze sana serikali, pia nimpongeze Mhe. Waziri lakini kubwa zaidi nataka nimpongeze sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Kwa kweli katika ripoti zote tena miaka yote, lakini safari hii ripoti zenyewe zinajieleza, yaani kwa kila aliyepata ripoti hizi na kwa bahati mbaya tumezipata asubuhi hii ya leo na kama tungezipata siku moja kabla, basi naamini Waheshimiwa Wajumbe wangekuwa na maswali mengi sana ya kuuliza. Lakini kimsingi ripoti zinajionesha ziko wazi tena ni ripoti ambazo zimekamilika.

Mhe. Spika, naomba uniruhusu kabla sijenda kwenye maswali, kwanza nipongeze katika hiki kitabu kimoja kuhusu Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Miradi ya mwaka 2009/2010. Mmoja miongoni mwa miradi ya wananchi uliojionesha katika ripoti hii ni mradi wa Skuli yangu ya Maandilizi ya Mkele. Kwa hivyo, inaonesha mpaka na mimi ninakaguliwa na hii inaonesha uwajibikaji mkubwa kwa watendaji wetu. Kutokana na hali hiyo, tunampongeza sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Vile vile nataka nimpongeze kwenye kitabu chake chengine cha Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu, Udhibiti na Uhifadhi wa Mali za Kudumu za Serikali ya mwaka 2009/2010. Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 48 kitabu hiki chenye picha za Mali za Serikali.

Kwa kweli kitu ambacho kimenisikitisha kwenye ukurasa wa 48 kumepigwa picha baadhi ya vyombo vya moto vya Mahakama ambavyo havifanyikazi kwa muda mrefu. Miongoni mwa vyombo hivi kuna kimoja kinaonesha ni kipya kabisa. Kutokana na hali hiyo, labda hapa Mhe. Waziri aje atupe maelezo, kwa nini vyombo hivi tena viko kwenye chombo cha kutoa maamuzi.

Katika ukaguzi yeyote atakayekosea anapelekwa mahakamani kwa ajili ya kuhukumiwa, lakini wao wenyewe ambao wanaosimamia kutuhukumu sisi, basi wao tayari kuna ajibu zao ambazo zimeoneshwa kwenye kitabu.

Sasa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, aje anijibu swali langu kwenye ukurasa 48 ni kwa nini mpaka leo vyombo hivi na vyengine vinaonesha vipya kabisa bado havijatumika?

Swali langu jengine kwanza Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora amekiri na ameendelea kunung'unika pamoja na kulalamika, kwamba katika ukurasa wa 58 naomba kunukuu Mhe. Spika.

> Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu wa Udhibiti na Uhifadhi wa Mali za Kudumu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010 ukurasa wa 58 unaeleza hivi:-
>
> "Ukaguzi umebaini kwamba wizara haina Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu, hii ni kwenda kinyume cha kifungu Nam. 264 cha Kanuni za Fedha za Zanzibar mwaka 2005. Aidha hali hii huweza kusababisha upotevu wa mali hizo".

Mhe. Spika, kuna sababu gani mpaka leo bado serikali inaendelea kulalamika kupitia Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa kweli hii inaonesha hata sisi Kamati zetu Baraza la Wawakilishi bado hazijawajibika vya kutosha, kwa sababu ripoti hii haigusi wizara moja isipokuwa inagusa wizara zote, tena Mhe. Spika umetupangia majukumu kwa wizara zote kwa ajili ya kuzisimamia utekelezaji wake.

Sisi kama tunavyoitwa ni *watchdog* kwa jina la kigeni, yaani mbwa wakali ambao wanaona na halafu wanaikemea serikali. Mhe. Spika, inaonesha hata Kamati zako za Kudumu za Baraza la Wawakilishi bado haziwajibiki. *(Makofi)*

Swali langu lipo hapa je, mapungufu haya yote ambayo yaliyotajwa kwenye ukusara wa 58 mpaka 59 katika kitabu hiki yatamalizika lini. Mhe. Spika, tunaona kwamba kuna baadhi hasa ya wawekezaji wanapohitaji kwa mfano maeneo basi mpaka taratibu za kiserikali zinavunjwa wa kwa ajili ya kupatiwa haya maeneo na ushahidi wakati mwengine tunao.

Lakini inapokuja *assets* za mali za serikali ambapo ukiangalia hata maeneo mengi hayakupigwa kwenye picha humu. Kwa mfanao, majengo ya wizara, mashamba ya serikali, yaani kuna maeneo mengi mpaka leo bado serikali haijayatambua kwamba hizi ni mali zake.

Sasa je, serikali inatuambia vipi, ili kuhakikisha kwamba katika ripoti inayokuja au kwenye bajeti inayokuja ya mwaka ujao Mhe. Waziri atakuja na ripoti gani ya kutuhakikishia mambo haya ya Mhe. Waziri kulalamika, Kamati ya *PAC* kulalamika pamoja na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kulalamika yatamalizika lini?

Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Kwanza naomba nianze kwa ruhusa yako kuungana na wenzangu kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la

Mji Mkongwe kutoa mkono wa pole kwa kifo cha Mjumbe wenzetu, ambaye pia alikuwa ni Mjumbe mwenzangu kwenye Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, marehemu Mhe. Mussa Khamis Silima pamoja na mkewe ambacho kilitokea katika ajali mbaya kabisa wakati walipokuwa wakielekea Dodoma.

Kwa hivyo, tunamuomba Mwenyezi Mungu awalaze marehemu mahala pema peponi, awape subira wafiwa na sisi atujaalie hatima njema.

Mhe. Spika, pia nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Mji Mkongwe kutoa mkono wa pole kutokana na msiba mkubwa uliolikumba taifa letu usiku wa tarehe 9 kuamkia tarehe 10 mwezi wa Septemba wa ajali mbaya ya Mv. *Spice Islander I* ambayo ilisababisha mamia ya Wazanzibari kupoteza maisha yao.

Kutokana na hali hiyo, tunatoa mkono wa pole pia vile vile tunawaombea Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema peponi na awape subira wafiwa wote pamoja na Wazanzibari kwa jumla, kwa sababu ulikuwa ni msiba wa taifa.

Kwa kweli ni imani yetu tukio hili litakuwa ni funzo kwetu kama nchi pia ni imani yetu kwamba kamati iliyoundwa kama ilivyoelezwa hapa kupitia taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*, kwamba ripoti yake itawasilishwa katika Baraza hili na kupewa nafasi ya kutosha kwa Wajumbe wako kujadili, ili kuona hatua gani zinapaswa zichukuliwe dhidi ya yote waliohusika na ajali hiyo.

Baada ya hayo Mhe. Spika, sasa naomba niende moja kwa moja kwenye shughuli ambayo tunayo hapa mbele yetu, ambayo ni kuuliza maswali kuhusu ripoti hizi tatu ambazo tumewasilishiwa hapa.

Mhe. Spika, sitaki kuwa mwizi wa fadhila naomba nipongeze kijumla, kwa sababu fursa ni ya maswali sio ya kujadili. Kwa hivyo, kwa jumla naipongeza Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri walioifanya na kutuwasilishia ripoti hizi nzuri ambazo ziko mbele yetu. *(Makofi)*

Vile vile niipongeze serikali na hasa Mhe. Rais kwa kuchukua uamuzi wa haraka wa kuagiza ziletwe mbele ya Baraza lako, ili ziweze kuchukuliwa hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, maswali yangu ni haya yafuatayo. Kwanza kwenye ripoti ya jumla ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 imebainisha mapungufu mengi. Lakini moja wapo kuna baadhi ya taasisi za serikali pamoja na mashirika yake nyengine hazikufunga hesabu za mwaka, nyengine hazikuwasilisha hesabu zake kwa ajili ya kukaguliwa nazo.

Kwa mfano, Baraza la Manispaa Zanzibar ambalo hata halikufunga hesabu zake, pia kuna Shirika la Utalii Zanzibar, *ZSSF*, *ZRB*, yaani hii Mamlaka ya Mapato inayotukusanyia mapato yetu, basi yenyewe haikuwasilisha hesabu zake kwa ajili ya kukaguliwa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pia Benki ya Watu wa Zanzibar pamoja na taasisi nyengine.

Sasa Mhe. Spika, nataka kumuuliza Mhe. Waziri kwamba serikali inachukua hatua gani kwa taasisi kama hizi, ambazo zinashindwa kufunga hesabu zake au kama zimefunga zinashindwa kuziwasilisha katika chombo hiki muhimu katika nchi yetu kwa ajili ya kukaguliwa, ili kuona fedha za walipakodi zinalindwa na zinatumika vile ambavyo zimekusudiwa? Hilo ni swali langu la kwanza.

Swali la pili Mhe. Spika, kumekuwa na kitu ambacho kinajirejea katika ripoti za kila mwaka, nacho ni hiki cha kutokuwepo kwa Daftari la Mali za Kudumu za Serikali au Zisizohamishika, lakini suala hili limekuwa likijirejea kila mwaka.

Jengine ni suala la wizara, mashirika, taasisi pamoja na idara kutokuwa na *Procurement Plan*, yaani Mpango wa Manunuzi kwa mwaka na matokeo yake inasababisha kuwa na manunuzi holela kama ilivyoripotiwa kwenye ripoti hizi. Vile vile suala hili limekuwa likijirejea katika ripoti takriban za kila mwaka za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, baya zaidi kuna taasisi kwa mfano kama Kamisheni ya Utalii, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na hata Chuo cha Maendeleo ya Utalii hawana hata Vitengo vya Manunuzi ambapo ni kinyume na Sheria ya Manunuzi ya nchi.

Kwa hivyo, naomba kujua kutoka kwa Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, serikali huwa inachukua hatua gani wakati inapopokea ripoti hizi na baada ya Baraza la Wawakilishi kutoa maelekezo yake? Kwa kweli tunapoona vitu kama hivi vimekuwa vinajirejea kila mwaka ni kuonesha kama vile alivyosema Mhe. Rais kwamba ni *business as usually*, kuwa tunafanya ukaguzi lakini baadaye tunaziweka kwenye makabati katika ofisini zetu na wala hazichukuliwi hatua yoyote, kwa sababu kama zinachukuliwa hatua basi yasingekuwa yanajirejea kila mwaka.

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri anisaidie kupitia kwako Mhe. Spika, kwa nini tunaendelea kuona matokeo haya kwa taasisi zile na yanajirejea kila mwaka na wala hatuoni *improvement* katika maeneo haya kama tulivyoona kwenye maeneo mengine?

Swali la tatu Mhe. Spika, naomba kujua kwenye ile Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu ya Udhibiti wa Ukaguzi wa Mali za Serikali ulikuwa na orodha ya wadaiwa wanaoishi kwenye Nyumba za Serikali. Sasa nimetizama mwaka huu na kulinganisha na mwaka jana sijui kama Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeona kwamba hatuna haja ya kuendelea kuwa nayo, kwa sababu hapa nimeona zaidi kuna nyumba ambazo ziko katika eneo la Mji Mkongwe.

Katika ripoti ya mwaka jana tulikuwa na ripoti yote kamili ya Nyumba za Michenzani, zilizoko mashamba Unguja na Pemba zilikuwa zikionekana na kulikuwa na wadaiwa sugu wengi. Kwa nini ripoti ile mwaka huu hatukuiona na tumeona nusu kwa eneo fulani tu, wale wadaiwa wakiwemo viongozi wakuu wa serikali na wengine ni Waheshimiwa Mawaziri katika Baraza lako hili, ambao wametajwa kwenye ripoti ya mwaka jana?

Serikali imechukua hatua gani kuona kwamba wanalipa na kufuata mfano mwema wa Mjumbe wako mimi ambaye ninalipa kila mwaka katika nyumba ninazoishi za serikali. *(Makofi)*

Mhe. Spika, swali langu jengine linahusu ripoti hizi kwa jumla, kwa sababu nimekuwa nikizifuatilia tangu niingie katika Baraza hili. Kwa kweli sijaona ukaguzi ambao unaelezea misamaha ya kodi katika nchi yetu Mhe. Spika. Moja kati ya maeneo ambayo mara nyingi mapato ya serikali yanavuja kupita kiasi na serikali inapoteza mapato mengi ni katika eneo hili la misamaha ya kodi, inayotolewa kwa mujibu wa sheria mbali mbali hasa katika Mamlaka ya Uwekezaji Zanzibar na hili silioni.

Mwaka jana nakumbuka nilipekua sana katika ripoti tuliyokabidhiwa mwanzoni mwaka huu sikuliona na mara hii pia nimetizama humu silioni. Kwa nini afisi hii inashindwa kutuletea ripoti au serikali ina siri gani katika suala la misamaha ya kodi na ushuru unaotoa, kiasi ambacho Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali wamekuwa hawafiki na kuweza kutupatia ripoti?

Mwisho kabisa swali langu kama alivyozungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, ukitizama hiki kitabu cha Ripoti ya Ukaguzi Yakinifu sehemu kubwa Mhe. Mjumbe alizungumzia vyombo vya moto vya Mahakama, lakini ukitizama kuna vyombo vya moto vingi sana kama vile magari, vespa, pikipiki, yaani kila sehemu ukifungua unakuta vitu hivi.

Suala hili Mhe. Spika, limekuwa ni tatizo kubwa sana katika nchi yetu, kwa sababu vyombo hivi matumizi yake tunaviona barabarani na hizi ni fedha za walipakodi kiasi katika matumizi yake tunayaona mpaka vinafanya binafsi ndio vifikie kuwa katika hali kama hii.

Sasa swali langu Mhe. Spika, kwamba serikali inachukua hatua gani na nani hasa mwenye kuhusika kusimamia udhibiti wa vyombo hivi? Je ni Wizara ya Utawala Bora, kwa sababu Utawala Bora ni *cross cutting* ama ni nani? Je, ni Wizara ya Fedha inayosimamia Mali za Serikali na inachukua hatua gani, kuona vyombo hivyo ambavyo vimejaa kwenye mahala, kama vilivyoonekana humu na baadhi yetu tumevishuhudia tulipokuwa tukitembelea katika kazi za kamati mbali mbali, vinafanyiwa matengenezo na kama vimekuwa havifai tena basi vinauzwa, ili fedha za walipakodi zisiendelee kupotea.

Mhe. Spika, nakushukuru naomba maswali yangu yajibiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nami nakushukuru kunipa nafasi hii naomba nimuulize Mhe. Waziri maswali yafuatayo. Kutokana na ripoti hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Spika, naomba kujua, kwa sababu tumekuwa tukipokea Ripoti ya *CAG* na hatimaye *PAC* tangu Baraza hili lilipoanza, tumekuwa tukidai hatua ambazo serikali ingechukua kila ripoti ya *PAC* inapokuja.

Namuomba Mhe. Waziri anifahamishe kupitia kwako Mhe. Spika, kuna kuwa na vikwazo gani vya kisheria ambavyo vinamkwaza au serikali vinaikwaza, ili hatua za kinidhamu zisichukuliwe kwa wale watendaji, ambao dhahiri wamekiuka Taratibu na Sheria za Utumishi hasa katika Sheria ya Fedha na Ununuzi?

Swali la pili, ripoti hizi zimeonesha kwamba kuna uzoefu mkubwa katika masuala mazima ya mikataba, ukodishwaji wa majengo pamoja na mali za serikali. Mhe. Spika, kwa kuwa *CAG* ameliona hilo na pia Baraza hili limekuwa likisema kila siku. Kwa hivyo, serikali itachukua hatua gani sasa kufuta mikataba yote ambayo *CAG* amethibitisha kwamba imefungwa kinyume na utaratibu na wala haikuzingatia masharti ya Sheria ya Zanzibar? *(Makofi)*

Swali jengine, kwa kuwa *CAG* pamoja na watendaji wake ni ofisi muhimu sana na kwamba kazi zao hufanywa sana na Kamati ya *PAC* na pia hivi sasa wanaingia kwenye Ukaguzi wa *Value for Money*. Je, Mhe. Waziri atafanya nini sasa kuwawezesha sambamba *CAG* ofisi pamoja na *PAC* kupata ujuzi wa mafunzo haya ya Ukaguzi Yakinifu, ili Ripoti ya *CAG* ipate mchango mkubwa kwa upande kwa Kamati ya *PAC*?

Mwisho kabisa Mhe. Spika, nimuulize Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwenye vitabu hivi tumeona kuwa kuna ucheleweshwaji wa Ripoti za Fedha za mwisho wa mwaka.

Ingawa nichukue nafasi hii kupongeza sana Ofisi yetu ya Baraza la Wawakilishi, kwa kweli hapa imevuka mtihani na nichukue nafasi hii kumpongeza Katibu wa Baraza pamoja na kamati yake nzima, kwamba sisi udhaifu huu hatukonao. Kutokana na hali hiyo, nawashukuru sana watendaji wa Baraza la Wawakilishi kwamba sisi tunawasilisha ripoti hii ya fedha kwa mwaka tena kwa wakati, pia napenda kuchukua nafasi hii kumwambia katibu aendelee.

Lakini naomba nimuulize Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, kwa kuwa kimekuwa ni kilio cha miaka yote, basi naomba kujua kwa wale watendaji ambao hawawasilishi ripoti ya mwaka ya matumizi hasa nini wajibu wao mbele ya serikali?

Mhe. Ali Abdalla Ali: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali machache ambayo mengine wameshauliza wenzangu. Lakini kabla sijauliza maswali yangu na mimi niungane na wazungumzaji wa mwanzo kutoa pole kwa kifo cha Mhe. Mussa Khamis Silima ambaye ni Mjumbe katika Kamati yangu ya Katiba, Sheria na Utawala, naiomba familia iwe na roho ya subira, kwa sababu hiyo ni mitihani ya Mwenyezi Mungu na kila mtu aliyeumbwa inaweza kumkuta.

Vile vile kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Mfenesini nitoe pole kwa serikali kwa msiba mkubwa wa kuzama meli, ninaziomba familia zote ziwe na subira na hiyo ni mitihani ya Mwenyezi Mungu tuipokee kwa sababu sisi ni wanadamu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo sasa nije kwenye kitabu cha Ripoti ya Mdhibiti ukurasa wa 7 kuhusu Madeni ya Serikali. Kwa kweli nimesoma taarifa imesema kwamba madeni ya ndani yamepungua kwa asilimia 2, lakini madeni ya nje yamezidi kwa asilimia 7.2. Kutokana na hali hiyo, naomba kupata maelezo ni kwamba je ni kitu gani kinachosabisha madeni ya nje kuzidi kama ipo sababu ya msingi basi tuelezwe tujue?

Swali jengine nizungumzie kuhusu suala la *TASAF* tunaishukuru serikali pamoja na wadau wa maendeleo kwa kusaidia wananchi kwenye mikoa mbali mbali katika miradi ya *TASAF*.

Mhe. Spika, suala la kusikitisha ni kwamba awamu ya kwanza ya miradi ya *TASAF* iko miradi bado haijakamilika na tuliposhauri itiwe katika awamu ya pili kwa ajili ya kuweza kukamilika imeshindikana. Kwa kweli hadi hivi sasa ninavyozungumza miradi ya awamu ya kwanza mingine bado haijesha. *(Makofi)*

Kwa hivyo, naiomba wizara kupitia kwako Mhe. Spika, kama kuna utaratibu wa kusaidiwa miradi hiyo, basi tuelezwe ili tukatoe maombi yetu kwa ajili ya kuweza kusaidiwa? Hilo swali la pili.

Swali la tatu kuna *querry* ambazo zinajirudia mara kwa mara kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa hiyo, naomba kujua *querry* kama hizi ambazo zinajirudia kitaratibu ama kisheria zichukue muda gani ziweze kufutwa kwenye vitabu?

Swali la mwisho kuhusu Miradi ya Maendeleo au Wananchi. Mhe. Spika, tunashukuru kwamba serikali ilikuwa na mfuko imetenga maalum kwa ajili miradi ya wananchi. Lakini kwenye bajeti iliyopita safari hii tumetoka kwenye miradi ya wananchi tumekuja kwenye Mfuko wa Jimbo, sasa kuna muda wa mpito na miradi ile mingi imesita.

Je, katika muda huu wa mpito kwa ajili ya kusubiri Mfuko wa Jimbo na huku Mfuko wa Miradi Midogo Midogo umefutwa, tufanye vipi ili miradi hii tuweze kuimaliza kabla haijaleta athari yoyote?

Nakushukuru Mhe. Spika ahansate sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza maswali kuhusiana na Ripoti hii ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwanza nimshukuru sana Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri anayoifanya yeye pamoja na timu yake ya watendaji, yaani ushirikiano wao ninaouona pale. Kwa kweli leo tunaona matunda ya ushirikiano ule kwamba tumepokea ripoti tatu kwa pamoja, ripoti zinazoonesha namna gani ya watendaji wetu kule serikalini wanayoyafanya.

Mhe. Spika, swali langu linakuja kama maoni hivi kidogo kuhusu suala la muda wa kazi wa Kamati ya *PAC*, kwa sababu tunaona namna gani hapa kwenye ripoti ya Mhe. Mwenyekiti jinsi alivyozungumzia *speed* aliyonayo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, yaani *speed* yake ni kubwa sana, kwa sababu leo tumepokea ripoti tatu na alisema kule iko moja na jumla zitakuwa nne. Lakini tukiangalia ule muda wenyewe wa kazi, yaani Kamati ya *PAC* inafanyakazi kama kamati nyengine za kisekta.

Kwa hivyo, naomba suala tulifanye marekebisho kidogo na kutokana na hali hiyo, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Spika, atusaidie ni utaratibu gani atakaotumia hasa kuweza kuiwezesha hii Kamati ya *PAC* ikaweza kufanyakazi zake kulingana na zile ripoti ambazo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo anazitoa, ili tukafuatana nao pamoja?

Ikiwa hivyo sivyo, itakuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yuko Darajani na sisi ndio kwanza tupo jengoni hapa ndio kwanza tunataka kuondoka na tunakokwenda bandarini,

sasa itakuwa mwenzetu anafika na sisi tuko mbali sana. Kutokana na hali hiyo, naomba kidogo Mhe. Waziri aje atusaidie kupitia kwako Mhe. Spika, namna gani anaweza kutusaidia, ili kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba katika hilo?

Jambo jengine Mhe. Spika, kuna suala zima la ukaguzi wa Taasisi za Muungano ambazo zinafanyiakazi hapa Zanzibar. Kwa kweli suala hili limekuwa kila baada ya muda tunapopata hizi ripoti huwa tunaliulizia ni lini Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atakuwa anazikagua taasisi zile, kwa sababu tunapata majibu tofauti. *(Makofi)*

Sasa namuomba Mhe. Waziri atueleze kupitia kwako Mhe. Spika, imefikia hatua gani kwa sababu tulizungumza naye hapa katika ripoti iliyopita na tulikubaliana kwamba suala hili litashughulikiwa. Kwa hivyo, namuomba atakapokuja atueleze amefikia wapi katika hili kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar anazikagua Taasisi za Muungano ambazo zipo hapa, kwa sababu jambo lile si suala la muungano?

Swali jengine Mhe. Spika, ni hatua gani zinazochukuliwa juu ya kuiwezesha Kamati ya *PAC* kujiunga na Jumuia tofauti nyengine za kisekta kama hii ambazo ziko huko duniani. Kwa mfano, kuna *South Africa Development Community Organization of Public Account Committee (SADCOPAC)* pamoja na nyengine. Sasa Kamati yetu hii ya *PAC* bado haijaingia sana kwa sababu ya mambo tofauti?

Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja atusaidie kupitia kwako Mhe. Spika, atueleze ni lini Kamati hii ya *PAC* itakuwa katika jumuia kama zile?

Ahsante Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nadhani tumefikia pahala pazuri kwa sababu yapo maswali yanayohusu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, pia yapo maswali yanayomhusu Mhe. Waziri aliyewasilisha ripoti hii. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena kunipa fursa pamoja na nafasi ya kuja kutoa ufafanuzi juu ya maswali na michango iliyotolewa na Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* pamoja na maswali, ambayo yameulizwa na baadhi ya Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, baada ya kuzipokea ripoti tatu ambazo hivi punde niliziwasilisha.

Kwanza naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wote ambao wameweza kupitia kwa haraka vitabu vyetu vitatu vya ukaguzi, kwa kipindi cha mwaka 2009/2010 na akaweza kupata masuali ya kuweza kutuuliza, hii ni kuonyesha kwamba waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wanao uwezo wa kuweza kuzipitia ripoti na kujua nini hasa ambacho kimekusudiwa katika ripoti hizo.

La pili nichukue nafasi hii kupokea pongezi kwa niaba ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali ambaye kwa taratibu zetu yeye hawezi kuvuka *red carpet* ile kuja kushukuru. Lakini naomba nichukue nafasi hii kwa niaba yake au kwa niaba ya Ofisi ya Mdhibiti na kwa

niaba ya serikali kwa jumla nipokee pongezi hizo ambazo Waheshimiwa Wajumbe wametupongeza.

Mhe. Spika, namshukuru sana Mhe. Mwenyekiti, wa kamati ya *PAC* kwa maelezo yake na michango yake ambayo ameeleza katika hotuba yake, Kamati ya PAC na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, zitakapoendelea kama zinavyofanya kazi kufanya kazi kwa mashirikiano makubwa ndipo eneo moja la uwajibikaji kwa watumishi wa umma na wengine wote wanaowatumikia wananchi tukiwemo sisi wawakilishi wa wananchi ndipo itakapotimia azma ile ya uwajibikaji.

Kwa hivyo niipongeze Kamati ya *PAC* kwa hilo na mimi kupitia Ofisi ya Mkaguzi nitahakikisha lile ambalo limo ndani ya uwezo wetu kama serikali tunalifanya kwa kushirikiana na Ofisi ya Baraza la Wawakilishi na Ofisi nyengine ambayo kwa leo naiwakilisha mimi kwa niaba ya Makamo wa Pili wa Rais kuona kwamba kamati ya PAC inapata muda kwa kushirikiana kufanya mazungumzo ya pamoja kati ya uongozi wa Baraza na Wizara yangu, Wizara ya Fedha pamoja na Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais. Umuhimu wa kupata muda zaidi kamati ya *PAC* upo na hasa tukilinganisha kwamba vitabu hivi ni vingi na ni kweli.

Mhe. Mwenyekiti, na wengine waligusia kwamba pengine ripoti ya Mdhibiti inaweza ikaja mwakani, nataka niwahakikishie kama itakuwa tayari wiki ijayo basi kikao kinachofuata tutaileta Barazani, wala hatutosubiri mwakani na tunafanya hivyo kwa sababu ya kuondosha usumbufu ambao umelalamikiwa na waheshimiwa wajumbe. Kwa muda mrefu imekuwa ripoti za nyuma ndizo zinazokuja na hata ukiangalia michango ya wajumbe hapa kwa sababu hizi ripoti zinatoka leo inaonyesha kama kwamba haya mambo yanafanyika sasa, lakini nakubali yapo mambo ambayo yanaendelea lakini yapo mambo ambayo kwa kiasi kikubwa ambayo yameripotiwa humu yalifanyika katika kipindi kilichopita. Lakini kwa sababu ya uchelewaji wa uwasilishwaji wa ripoti ndipo tunapata wasaa wa kuweza kuyazungumza haya.

Kwa hivyo katika kukabiliana na hilo tutajitahidi ripoti tuwe tunakwenda na kipindi cha mwaka wa fedha wa mwaka kama sheria inavyotutaka, kwa hivyo nimshukuru sana Mhe. Mwenyekiti, wa kamati kwa kutoa maelezo na ushauri nataka nimuahidi kwamba tutashirikiana kupitia ofisi ya Mdhibiti ili kuhakikisha kwamba na wao wanapata fursa ya kufanya kazi zao vizuri.

Mtu wa pili alikuwa ni Mhe. Hamza Hassan Juma ambaye ameuliza masuali matatu, lakini moja alikuwa anasema nilipokuwa nikiwasilisha kama kwamba nilikuwa nikilalamika. Nilikuwa silalamiki nilikuwa natimiza wajibu wangu katika kutekeleza utaratibu wa uwajibikaji kueleza kilichopo silalamiki wala sinung'uniki na natoa rai kwamba sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tusilalamike bali tushauri, tutoe rai juu ya yale ambayo tunayaona ili serikali iweze kuyafanyia kazi.

Mhe. Hamza Hassan Juma aliuliza suala la vyombo ambavyo vimeonyeshwa katika vitabu na akaitaja taasisi moja muhimu sana katika nchi hii, ni sehemu ya muhimili mwengine wa nchi hii kwamba vyombo vile kwa nini vipo pale. Nataka kusema katika nchi katika watendaji katika watumishi wa umma hakuna ambaye yuko juu ya sheria, ndio maana Mdhibiti ameonyesha vyombo vile vilioko katika chombo hicho kikubwa sambamba na taarifa iliyoeleza juu ya sisi kufuata utaratibu kama Baraza la Wawakilishi kufunga mahesabu kwa wakati. Kama tungekuwa

hatukufunga mahesabu kwa wakti mdhibiti pia angetueleza. Huu ndio utaratibu wa uwajibikaji kwenye misingi ya kufuata utawala bora tunaeleza mambo kwa uwazi, tunatakiwa kushauri mambo kwa uwazi.

Kwa hivyo si suala la nani kafanya kosa, suala la kwamba mtu kafanya kosa basi sheria itafuata mkondo wake awe Waziri wa Utumishi wa Umma awe mwengine, sheria itafuata utaratibu kwa mujibu wa hali halisi ilivyo, sisi tulichofanya tumeripoti kwa yale mambo ambayo tumeyaona. Mapungufu haya yataondoka lini ambayo inaonekana hakuna udhibiti wa mali za serikali.

Madhumuni ya Mkaguzi kuchunguza mahesabu na mambo mengine yote yanayohusu mambo ya fedha na mali ni kuionyesha serikali mapungufu yaliyopo. Madhumuni ya ripoti hii kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu ni kwamba kamati ya PAC nayo ina nafasi yake ya kwenda kuyaona na hatimaye iweze kuishauri serikali. Kwa hivyo serikali itakabiliana na yale yote ambayo Baraza hili tukufu itayaonyesha kwamba ni mapungufu na ripoti ya mdhibiti itakapoonyesha kwamba ni mapungufu basi serikali inawajibika kuweza kuyaondosha mapungufu hayo hatua kwa hatua, tunakiri kwamba mapungufu ni mengi lakini hivi sasa tumedhamiria kuyaondosha mapungufu hayo.

Vipi tutaondosha mapungufu haya tunaondosha mapungufu haya kwa sababu hivi sasa serikali tumejiwekea utaratibu wa kuweza kuzipokea hizi ripoti na kuzifanyia kazi, pia na ripoti za kamati za Baraza la Wawakilishi kwa jumla. Lakini yanayohusiana na mapungufu yaliyoonyeshwa na mdhibiti sambamba na ile ripoti ya *PAC*. Kwa hivyo tumeanza kazi hiyo na tutajitahidi kuona kwamba mapungufu hayajirejei, lakini mapungufu yakiendelea kuwepo maana yake utawala wa kidunia umewekwa kwa ajili ya kuchunga watu au wanadamu na kama wanadamu tupo yatajitokeza mapungufu, lakini ikitokezea Haji .Omar Kheir kafanya pungufu hili leo na kesho anarejea tena na kesho kutwa anarejea tana hilo hukumu yake itakuwa ni nyengine.

Lakini kusema unaondosha kabisa mapungufu nafikiri mapungufu yataendelea kuwepo madhali utawala wa kidunia unaoongoza wanadamu upo. Kwa hivyo nataka nimhakikishie Mhe. Hamza kwamba serikali mapungufu itakabilana nayo hatua kwa hatua na tutajitahidi sana tuweze kukabiliana na mapungufu hayo ili yasijirejee katika ripoti zinazokuja.

Mhe. Spika, mtu wa tatu alikuwa ni Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye na yeye ameuliza masuala na amesema serikali inachukua hatua gani kwa taasisi zilizoshindwa kufunga hesabu. Kwanza hii sio hiyari huu ni utaratibu wa kuwajibika, kwa hivyo kwa zile taasisi ambazo hazikufunga mahesabu serikali itahakikisha inazihimiza ili iweze kufanya wajibu wake hiyo ni hatua ya mwanzo.

Lakini kama nilivyosema ikionekana pengine kama mahesabu haya hayakufungwa kwa sababu ya kukwepa maovu basi hatua za kisheria zitachukuliwa juu ya watendaji wa taasisi hizo, taasisi kutokuwa na *fixed asset register,* hili ni jambo ambalo sasa hivi tumelidhamiria na lazima liwepo. Katika bajeti iliyopita Mhe. Waziri wa Fedha aliulizwa masuala haya na Baraza lako tukufu Mhe. Spika, lilieleza, nataka niwahakikishie wajumbe kwamba hatukuishia hapa tulikaa serikalini na kuzingatia haya maoni yaliyotolewa na Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu la Wawakilishi na pengine hatua kwa hatua pengine kamati zitakapokwenda sasa katika

taasisi mbali mbali zinaweza kuona kwamba hali ilivyokuwa pale mwanzo na hali ilivyo sasa kuna tofauti kidogo.

Sasa hivi kila mmoja angalau analizungumza hili la *fixit asset register*. Kwa hivyo nataka nimhakikishie Mhe.Ismail Jussa Ladhu kuwa serikali imechukua hatua na nyinyi wenyewe hatuna haja ya kujisifu piteni Mawizarani mtakwenda kuona au katika taasisi za umma, kwamba kuna tofauti kati ya kipindi kilichopita na hivi sasa.

Ripoti kwa nini haionyeshi madeni ya wadaiwa, kuna mambo mawili ripoti yoyote inahitaji kufanyiwa kazi lakini vile vile kwa zile taasisi zinazohusika pengine zitakuwa zinawasiliana na wanaodaiwa, ama watakuwa wamesawazisha madeni yao ama pengine kuna hatua nyengine za kiserikali za kuwachukulia hatua kwa kufanya makosa ambayo yameonekana katika ripiti iliyopita.

Ripoti ya misamaha ya kodi ya Serikali ina siri gani hata haionekani kwenye ripoti ya Mdhibiti, madhali misamaha ni pesa za umma ninachotaka kukuhakikishia kwamba tutalifuatilia hilo tunalichukua na ishalla pengine kwenye ripoti hii tunayokwenda nayo tutakapokuja nayo pengine unaweza kuona orodha ya misamaha ambayo imetolewa katika kipindi hiki. Hakuna siri yoyote ile misamaha inatoa mwanya wa kusamehe pesa za walipa kodi na pesa za walipa kodi ni pesa za wananchi kwa hivyo hatuwezi kuwa na usiri wa kuficha haki ya wananchi, ninachotaka kumhakikishia Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwamba hili nalo tunalichukua na ishaalla kwenye ripoti ya mdhibiti na mkaguzi kipindi kijacho unaweza kuona eneo ambalo litaonyesha misamaha ya kodi.

Vyombo vya moto nani anasimamia aliuliza pia suala hili, kwanza kila taasisi inawajibika katika kusimamia chombo chake cha usafiri kwa hivyo muwajibikaji ni yule anayekimiliki kile chombo, lakini kwa taarifa ya Baraza lako tukufu hivi sasa Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano kama nilivyoeleza kwenye bajeti tuko katika hatua za mwisho za kutengeneza sera ya usafiri. Kwa hivyo inaweza kujumuisha pengine na hizi, lakini katika suala zima la vyombo vya serikali hivi sasa viko chini ya Hazina na mali yoyote ya serikali inakuwa ni mali ya Hazina kwa niaba ya wananchi, kwa hivyo nalo hili kutokana na mapungufu yaliyojitokeza nadhani tunahitaji kujipanga ili tujue hasa nani anawajibika katika eneo hili.

Mheshimiwa mwengine alikuwa ni Mhe. Hija Hassan Hija kuna vikwazo gani vya kisheria kuwachukulia hatua wanaokiuka sheria, hakuna vikwazo taratibu zipo hakuna vikwazo, sheria zipo tutafuata sheria hakuna muhali katika kufuata sheria, kwa hivyo nataka nikuhakikishie kwamba hakuna vikwazo kwa sababu wewe umeuliza vikwazo ni taratibu tu ili uweze kumchukulia mtu hatua nadhani ziko taratibu ambazo zimeelezwa hizo ndizo zinazopaswa kuzingatiwa.

CAG kushauri kufuta baadhi ya mikataba, mimi nadhani kuna taratibu za kufuta madeni kwa ile mikataba ambayo itakuwa inaonekana ina matatizo sidhani kama kuna kikwazo cha *CAG* kumdhuia kuishauri serikali, itakapotokezea hivyo basi nadhani serikali itachukua hatua kwa hivyo hakuna kikwazo maana yeye anaishauri serikali juu ya alichokiona . Kwa hivyo katika kile alichokiona basi kuishauri serikali na serikali inapaswa kusikiliza ule ushauri hasa kwa vile kile

anachokishauri kinakuja kwenye Baraza la Wawakilishi na *PAC* nayo ina nafasi yake ya kushauri.

Kuwajengea uwezo watendaji wa *Cag na PAC* watendaji wa kadi kwenye bajeti yangu nilieleza na hata kwenye muhtasari wa ripoti yetu tumeeleza ni kwa jinsi gani sisi tunaendelea kuwajengea uwezo. Kwa hivyo hilo lipo ndani ya mamlaka yetu na nawahakikishia wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba tutaendelea kuwajengea uwezo watendaji wa kadi ili waendane na ukaguzi wa kisasa. Hivi sasa Alhamdulillah wale ambao Mhe. Spika, pale umewanyanyua naomba tena simameni ile safu iliyopo pale hakuna a,b,c,d nikisema hivyo mnanielewa, na kuna kama wale wengine wako ofisini na tunaotarajia kuwaajiri wenye koliti kama ile. Ahsanteni sana.

Kwa hivyo kwa upande wa *PAC* kama nilivyosema mwanzo maoni ya Mwenyekiti tumeyasikia Baraza lenyewe limesikia katika kupanga vipaumbele vya kamati ipi ina kazi zipi wakati upi, mimi nadhani hili Mhe. Spika, huna mgogoro nalo, Katibu huna mgogoro nalo na sisi pia hatuna mgogoro nalo, kwa hivyo tutajitahidi kushirikiana ili tuone *PAC* inafanya kazi zake ili kukidhi haja.

Watendaji ambao hawawasilishi ripoti nimeshaitolea ufafanuzi sina haja ya kuirejea tena, Mhe. Ali Abdalla Ali ni kitu gani kilichosababisha madeni ya nje yazidi kuliko madeni ya ndani, mimi nadhani hii inatokana na mikopo kutokana na maendeleo tunayoyahitaji haja ya maendeleo tunayohitaji sisi Wazanzibari, hivi sasa katika kipindi cha maswali na majibu kuliulizwa masuala ya barabara na kadhi iliyopo.

Kuna miradi mbali mbali katika nchi hii hasa hii miradi ya *TASAF* ni mkopo unaodhaminiwa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, lakini kuna mikopo ambayo inajenga uwanja wa ndege, kuna mikopo inajenga barabara hii ndio inayosababisha madeni ya nje yapande kuliko mdeni ya ndani. Kwasababu maendeleo tunayahitaji na uwezo wetu wa ndani kifedha kuyatekeleza hayo ni mdogo.

Miradi ya TASAF kwamba katika kipindi kilichopita kuna miradi ambayo haikukamilika katika ripoti yangu nilisema kwamba katika maeneo haya kuna mapungufu, kwamba miradi hii kwa *nature* yake wananchi wenyewe ndio wanatakiwa waiibue, sasa yapo mapungufu ambayo sisi kwenye vitabu vyetu vya ripoti tumeyaeleza. Nadhani serikali kwa upande wetu tukiweza kuyafanyia kazi mapungufu ambayo yamejitokeza katika miradi ya wananchi na miradi ya *TASAF* katika kipindi kijacho inaweza isijitokeze.

Suala la kuwa inasaidiwaje miradi ile mimi nadhani tusubiri mikakati ya Wizara ya Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais inaweza kutoa ufafanuzi kwa jinsi gani inaweza kusaidia hiyo, lakini ndio maana tumeonyesha mapungufu ili tuweze kukabiliana na mapungufu yaliyokuwepo.
Utaratibu wa kufuta *querry* umerejewa tena kule ilikuwa inazungumzwa kufutwa mikataba kwa ushauri wa mdhibiti, hapa limeulizwa suala la kufuta kwiri mbali mbali zinazokaa kwa muda nadhani kuna urataribu wake pale mdhibiti anapoona kwamba kwiri hii imekaa kwa muda mrefu haitekelezeki wala haijibiki, nadhani ziko taratibu ambazo mdhibiti anaishauri serikali au taasisi inayohusika kwa kuweza kuiondosha *querry* hiyo.

Mwisho alikuwa Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando yeye alieleza maelezo kwa sababu ni mjumbe wa *PAC* na maelezo aliyoyaeleza Mhe. Mwenyekiti, na Mhe. Hija Hassan Hija nimetoa ufafanuzi wa kutosha nadhani abaki na majibu yangu yale ambayo nimeyaeleza.

Lini Mkaguzi atafanya kazi kuzikagua taasisi za Muungano jambo hili linaendana na taratibu za sheria na kama linaendana na taratibu za sheria iko kazi serikali inatakiwa iifanye kati ya taasisi inayosimamia Sheria tulizoziweka kwa taasisi za Muungano na sheria ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu, kwanza tuzungumze tukubaliane hatuwezi tu leo na kesho tukamwambia mkaguzi wetu nenda lakini lazima tukubaliane kimsingi.

Katika hili hakuna matatizo kwa sababu mdhibiti anayo haki ya kufanya kazi za uwakala, kwa hivyo ni mazungumzo ninachoweza kusema ni kwamba bahati mbaya ni kwamba miongoni mwa mambo ambayo tulikuwa tumeyaweka katika *package* ya kwenda kuzungumza na wenzetu ni pamoja na kadhia hii, lakini kwa bahati mbaya katika ngazi ya Mawizara tumelimaliza sasa tunasubiri katika ngazi ya vikao vile vikubwa na ishaalla kwa sababu nia yetu ni njema ya kumtaka mkaguzi afuatilie haya sidhani kama wenzetu wanaweza kuwa na mashaka nayo.

Lakini tunahitaji mazungumzo, maelewano na hatimaye kwa yale maeneo ambayo tunayahitaji kurekebishiwa sheria basi tuweze kufanya marekebisho ama SMZ ifanye marekebisho ama SMT ifanye marekebisho na tuweze kutekeleza huu ushauri ambao tunapewa na waheshimiwa wawakilishi.

Kamati ya *PAC* kujiunga na taasisi za kimataifa hapa sijui alikusudia *PAC* au alikusudia *CAG* taratibu zinaendelea za kutaka wajumbe, lakini kama ni *PAC* maana yake ni Baraza nafikiri taratibu za Baraza kwenye mabunge ya Jumuia ya Madola na Mabunge mengine ya kidunia zipo zinazotuongoza katika kufanya kazi hiyo. Mhe. Spika, amelisikia na Katibu amelisikia nadhani ataweza kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, kwa pamoja niendelee kuwashukuru waheshimiwa wajumbe wote ambao wameuliza masuala na wale ambao hawakuuliza masuala najua pengine walikuwa nayo. Lakini kwa sababu ya muda hawakupata. Lakini kwa sababu tumewapa vitabu na kazi yetu sisi wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ni kufanya utafiti ili tuje tuishauri serikali juu ya yale ambayo tunayaona ni mapungufu vitabu hivyo mnavyo kaeni navyo ili vikuwezesheni kujenga uwezo wa kuishauri serikali vizuri.

Baada ya hayo siwezi kusema machache Mhe. Spika, ahsante sana nakushukuru na nawashukuru sana wajumbe kwa kunisikiliza. *(Makofi).*

Mhe. Spika: Nakushukuru Mheshimiwa Mjumbe na nawashukuru Waheshimiwa wajumbe sasa kazi iliyobakia ni ndogo ni kuipokea ripoti hii. Sasa niwahoji wanaokubali kupokea ripoti hii wanyanyue mikono, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Spika: Ripoti imepokelewa na iko tayari kufanyiwa kazi na kamati husika.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali

(Kusomwa kwa mara ya kwanza)

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naomba kukushukuru wewe kwa kuniruhusu kuwasilisha Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya Kuanzishwa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, ni faraja iliyoje kwamba baada ya miaka mingi kupita Zanzibar kuanzia sasa itaendesha shughuli zake za Mkemia Mkuu kwa utaratibu wa sheria iliyopitishwa na Baraza lako tukufu, na mimi kabla ya kuanza naomba niungane na wenzangu Wajumbe wa Baraza lako tukufu kutoa mkono wa pole kwa familia ya Muwakilishi mwenzetu, kifo chake kiwe ni tahadhari kwetu kwamba kifo ni siri ya Mwenyezi Mungu pekee na hivyo na sisi tujiandae kufanya mema na kusali ili tujitengenezee maisha ya baadaye.

Mhe. Spika, naomba pia niungane na wananchi wengine kutoa rambi rambi kwa msiba mkubwa uliotupata kwa Tanzania na hasa Zanzibar, kutokana na kuzama kwa meli ya MV. Spice Islanders I.

Mhe. Spika, mimi kama Waziri wa Afya nawashukuru na kuwapongeza wafanyakazi wa Wizara ya Afya kwa umoja wao na mshikamano wao mkubwa waliouonesha katika kukabiliana na tukio lile, kwa kuwahudumia na kuwapa tiba wale ambao walikuja katika hospitali zetu. Umoja ule umewapa moyo sana Wananchi wa Zanzibar walio wengi. Hasa wale waliopatwa na msiba ule.

Wizara ya Afya imepata heshima kubwa kutokana na jinsi tulivyoshikamana kuikabili shughuli ile ngumu tuliyokuwa hatukujiandaa wala hatukuitegemea. Madaktari wetu waliokuwepo Nungwi, madaktari wetu waliokuwepo pwani bandarini, madaktari wetu waliokuwepo hospitali ya Kivunge na hasa hospitali kubwa ya Mnazi Mmoja, walishikama bila ya kujali daraja zao za kazi.

Kwa taarifa ya Baraza hili hata wale madaktari waliokuwa wastaafu walishikama na sisi kuja kukabili suala lile. Naomba kutoa shukurani zangu kwa wananchi, wafanyabiashara, na wote waliosaidia tukafanikiwa tukafanya kazi ile.

Mhe. Spika, baada ya shukurani hizo, naomba sasa kuwakilisha muhtasari katika kuweka mbele ya baraza lako Mswada wa Sheria wa Kuweka Masharti ya kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, Rasimu ya Sheria ya Maabara ya Mkemia Mkuu ina madhumuni na lengo la kuanzisha sheria itakayohusu huduma ambazo zitatolewa na maabara ya Mkemia Mkuu ikiwa ni pamoja na kupima dawa za kulevya na kuangalia viwango vya chakula, dawa, kemikali, sumu na

vipimo vya *DNA* pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa serikali pamoja na jamii. Pia itawezesha kwenda Mahakamani kutoa ushahidi kuhusiana na uchunguzi wa maabara uliofanyika kwa kesi zinazohusiana na dawa za kulevya au kesi yoyote ile itakayohitaji utaalamu kwa Mchemia Mkuu pamoja uchunguzi wa *DNA*.

Naomba uniruhusu nishukuru Kamati ya Baraza lako Tukufu ya Ustawi wa Jamii, Wanawake na Watoto ambayo iliupitia Mswada huu na kutoa maelekezo, masahihisho kwa nia ya kuufanya uwe bora zaidi. Tulikaa na kamati hiyo kwa muda wa siku mbili na baada ya marekebisho leo tunauleta kwenu.

Mhe. Spika, maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa sasa imekuwa haina sheria. Ilikuwa inafanya kazi zake kwa kutumia dikrii na kuanzia kwake. Hivyo ilikuwa inakosa nguvu za kisheria. Pia ukosefu wa jengo rasmi la maabara imeelekea kushindwa kufunga mashine za kisasa ambazo hutoa ufanisi katika uchunguzi na kuchangia katika kutoa huduma bora. Itakapopitishwa sheria hii tutapata nguvu sasa ya kujiandaa kwa yote yale yanayostahiki na kupata kutoa huduma iliyo sahihi.

Madhumuni ya kutaka kuanzishwa kwa sheria hii ni kuifanya maabara ya Mkemia Mkuu kuwa ni wakala wa serikali na kuwa na nguvu ya kisheria katika kutekeleza majukumu yake.

Mhe. Spika, maabara ya Mkemia Mkuu ina umuhimu wa pekee kuwepo katika nchi ambapo mbali ya kuwa na majukumu ya kuangalia viwango vipya pia ina majukumu yafuatayo:-

1. Kutoa ushauri wa kisayansi kwa taasisi pamoja na jamii kuhusu ubora na usalama wa chakula, kuwepo au kutokuwepo sumu na chemikali katika chakula na bidhaa mbali mbali.

2. Kusimama ubora wa maabara zilizomo katika nchi.

3. Kupima pamoja na kutoa majibu kuhusiana na masuala ya *DNA*.

4. Kusimamia matumizi ya kemikali za viwanda na kemikali za matumizi ya kawaida, pamoja na kulinda afya ya jamii na mazingira.

5. Kutoa mafunzo kwa taasisi, viwanda na jamii kuhusiana na mambo yanayohusu chakula, dawa za kulevya, kemikali ya sumu.

Mhe. Spika, Mswada huu una makundi mawili.

Sehemu ya Kwanza:

- Inahusu mambo ya Utangulizi ambalo ni Jina la sheria na ufafanuzi wa baadhi ya vipengele.

Sehemu ya Pili:

- Inahusu kuanzishwa kwa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na kazi za maabara hiyo,
- Kuteuliwa kwa Mkemia Mkuu pamoja na majukumu yake.
- Kuteuliwa kwa Wachunguzi wa maabara wa serikali pamoja na majukumu yao.
- Kuanzishwa kwa bodi ya ushauri kazi zake na posho ambazo wanapewa wajumbe.
- Kuenguliwa katika majukumu kwa wajumbe wa bodi ya ushauri, afisa au muajiriwa, katika Maabara Mkemia Mkuu wa serikali ambaye atafanya au kuacha kitu kwa nia njema.
- Uhusiano baina ya maabara ya Mkemia Mkuu wa serikali na taasisi nyengine au mashirika.

- Utunzanji wa siri katika matokeo ya uchunguzi

Sehemu ya Tatu:

- Inahusu vifungu vya fedha,
- Mikakati ya utekelezaji katika maabara.
- Fedha na vyanzo vya maabara ya Mkemia Mkuu.
- Tathmini ya uingizaji matumizi na udhibiti wa fedha
- Hesabu na ukaguzi na ripoti ya mwaka itakayotayarishwa na Mkemia Mkuu wa Serikali.

Sehemu ya Nne:

- Inahusu masharti ya jumla ambayo imeeleza makosa ya adhabu.
- Uwezo wa Waziri kutunga Kanuni.
- Kufutwa kwa Sheria ya Chakula na dawa.

Matokeo ya kupitisha sheria hii ni mategemeo ya Wizara ya Afya. Mswada wa Sheria ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali utakapopitishwa utasaidia kwa kiasi kikubwa katika utendaji wa kazi kwenye maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, hususan katika kusimamia matumizi ya kemikali za viwanda na zile za matumizi ya kawaida. Pamoja na uteuzi wa wachunguzi wa maabara ambao hulazimika kwenda mahakamani kutoa ushahidi kutokana na uchunguzi wanaoufanya.

Mhe. Spika, waraka huu unapendekeza kuanzishwa kwa sheria mpya ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Hivyo Wizara ya Afya inaomba Baraza lako tukufu likubali mapendekezo haya ili kuipa nguvu za kisheria maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Kupatikana kwa sheria hiyo kutaiwezesha maabara kupata nguvu ya kununua vifaa vinavyostahiki na kutayarisha jengo lenye haiba na sura ya kitaalamu kwa Idara yenyewe. Pia kuwezesha kufanya shughuli zake kitaalamu.

Mhe. Spika, Wizara ya Afya inatanguliza shukurani zake za dhati tena kwa wajumbe wote na kuwaomba kuujadili waraka huu, kwa nia ya kuimarisha na kuifanya sheria ambayo inaweza kutekelezeka. Mhe. Spika naomba kutoa hoja.

Mhe. Ashura Ali Sharif (Kny/Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii): Ahsante sana Mhe. Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mwenyekiti wa

Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii, naomba kusoma hotuba ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusiana na mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuweka sheria ya kuanzishwa maabara ya mkemia mkuuwa serikali pamoja na mambo mengine yanayohusiano na hayo.

Mhe Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima wa afya. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwa msemaji wa mwanzo kuwasilisha maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake na Ustawi wa Jamii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti ya Kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

Mhe. Spika, aidha, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwajaalia afya njema wajumbe wa Baraza lako tukufu kuweza kukutana leo hii ili kujadili na hatimae kupitisha Mswaada huo wa sheria.

Mhe. Spika, shukrani zangu pia ziwafikie wajumbe wa Kamati, watendaji wa Wizara ya Afya pamoja na wanasheria wetu wa Baraza na Serikali kwa mashirikiano ya kutosha kwa kutoa mchango na kutupa muungozo na ufafanuzi wa baadhi ya mambo wakati wa kuupitia na kuuchangia Mswada hasa ukizingatia kuwa Mswaada huo unahitaji utaalamu mkubwa.

Mhe. Spika, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya Kamati yangu kutoa mkono wa pole kwa ndugu na jamaa wa marehemu Mhe. Mussa Khamisi Silima pamoja na wananchi wa Jimbo la Uzini. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema Peponi. Amin.

Naomba pia nichukue fursa hii kwa niaba ya Kamati yangu kutoa mkono wa pole kwa msiba wa kitaifa wa ajali ya kuzama kwa Meli ya Mv Spice Islander, iliyotokea mwezi uliopita na kuwaombea dua wote waliotangulia. Mwenyezi Mungu awape malazi mema Peponi. Amin.

Mhe. Spika, naomba niwataje wajumbe wa Kamati ambao walihusika katika kuupitia Mswaada huo.Wajumbe hao ni:-

1. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Mwenyekiti
2. Mhe. Hija Hassan Hija	Makamo Mwenyekiti
3. Mhe. Asha Abdu Haji	Mjumbe
4. Mhe. Ashura Sharif Ali	Mjumbe
5. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Mjumbe
6. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
7. Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
8. Mhe. Saleh Nassor Juma	Mjumbe
9. Nd. Talib Enzi Talib	Katibu
10. Nd. Asha Said Mohamed	Katibu

Mhe. Spika, Mswada huu unakusudia kutunga sheria ya kuanzishwa na kufanyakazi kwa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kazi zake pamoja na mambo mengine yanayohusina na hayo.Kazi za Maabara hiyo zimeelezwa kwa kina na Mhe. Waziri wa Afya katika hotuba yake.

Hadhi ya Maabara ni kuwa wakala wa Serikali na chombo kinachojitegemea katika kudhibiti viwango vya chakula, dawa, kemikali na bidhaa nyengine zinazolingana na hizo.

Mhe. Spika, katika kipindi cha Januari/March 2010/2011, wakati kamati yangu ikiwa katika kufuatilia utekelezaji wa kazi zake katika Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, ilibaini matatizo mengi yanayoikabili Maabara hii ikiwa ni pamoja na kukosekana kwa Sheria ya kusimamia chombo hiki muhimu katika nchi.

Hali hiyo Mhe. Spika, imechangia kwa kiasi kikubwa kukosekana kwa ufanisi katika Maabara hiyo ambayo ina wataalamu wazuri tena wazalendo. Kwa kweli Kamati yangu inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuanzisha Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kisheria.

Mhe. Spika, hata hivyo kamati yetu inaitanabahisha serikali kuondokana na urasimu usio wa lazima katika ucheleweshwaji wa kuanzisha vyombo au taasisi muhimu zenye mustakbali na maisha ya watu kisheria. Kama tunavyofahamu waheshimiwa wajumbe, Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ni chombo muhimu katika nchi ambacho kina jukumu la kuchunguza na kupima chakula kinachofaa kwa matumizi ya binadamu, dawa za kawaida, dawa za kulevya, kemikali na sumu na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na jamii.

Mhe. Spika, katika kuipa hadhi Maabara ya Mkemia Mkuu, kamati yetu inaishauri Serikali kuzingatia kwamba ofisi za Mkemia Mkuu, Bohari Kuu ya Dawa pamoja na Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi zinatengwa katika eneo moja maalum badala ya kuzichanganya na ofisi nyengine kama vile ofisi ya uchapaji ambayo haiendani kiutendaji. Hali hiyo itasaidia taasisi hizo kuweza kufanya kazi zake kwa karibu na kuleta ufanisi.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa niende katika mswada husika
Mhe. Spika, kimsingi kamati yetu imekubaliana na mapendekezo ya rasimu ya Mswada, hata hivyo imefanya baadhi ya marekebisho kwa lengo la kusaidia kuboresha Mswaada huo. Marekebisho hayo ni ya kimaandishi na yale ya msingi.

Mhe. Spika, naomba nieleze baadhi ya marekebisho ya msingi ambayo Kamati yetu inaona yangefaa kufanyika.

Mhe Spika, kwanza, Kamati inapendekeza katika ukurasa wa 242, katika kifungu cha 14(1), kinachoainisha wajumbe wa Bodi ya Ushauri ya Maabara, kuongezwa kifungu cha 14(h) kitakachomuainisha Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii kuwa nae pia ni mjumbe wa Bodi hiyo. Hii ni kutokana na kamati kuona kuwa kwa vile miongoni mwa kazi za Maabara hiyo ni kufanya au kuratibu uchunguzi wa vipimo vya *DNA* ambavyo huhitajika katika kesi nyingi za udhalishaji wa watoto ambapo Mkurugenzi wa Ustawi wa Jamii ndio msimamizi wake. Kamati inaona kuwa mjumbe huyo atasaidia katika kushauri na kujenga hoja katika kusimamia haki na maslahi ya watoto katika masuala ya vipimo hivyo vya *DNA*.

Mhe.Spika, aidha Kamati yetu inapendekeza katika ukurasa wa 244, kufanyiwa mabadiliko kifungu cha 21(1) kinachoainisha Fedha na Rasilimali za Maabara kuwa kifungu cha 21(2) na kuingizwa kifungu chengine cha 21(1) kitakachoainisha Kuanzishwa kwa Mfuko wa Maabara.

Mhe. Spika, mapendekezo hayo yametokana na kamati kuona kuwa katika kifungu cha 21 kulitajwa Mfuko wa Maabara ambapo hakikuanishwa kifungu cha kuanzishwa kwake.

Mhe. Spika, katika ukurasa wa 245 kifungu cha 24(1) kinachohusiana na Makosa na Adhabu, kamati imefanya marekebisho na kupendekeza faini isiyopungua shilingi milioni tatu na isiyozidi shilingi milioni tano ama kifungo kisichopungua miaka miwili na kisichozidi miaka mitano ili kutoa uhuru zaidi kwa hakimu katika kufanya maamuzi.

Mhe.Spika, mwisho, katika ukurasa 246, kamati yetu inashauri kuongezwa kifungu cha 25(h) ambacho kitampa uwezo waziri mwenye dhamana ya masuala ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kutunga kanuni zitakazoelezea aina za kemikali zitakazoruhusiwa kisheria kutumika katika matumizi ya kawaida na Kemikali za viwandani. Haja ya kuwepo kwa kanuni hii ni kutokana na Kamati yangu kuona kuwa bado jamii inaonekana kuendelea kutumia kemikali za viwandani kwa matumizi kinyume na taratibu na maelekezo ya kitaalamu.

Mhe. Spika, kamati yetu inaunga mkono Mswaada huu na inawaomba wajumbe waungane nasi kwa kutoa maoni kadri watakavyoona inafaa na hatimae kuunga mkono na kuupitisha Mswaada huu muhimu kwa malahi ya taifa letu.

Mhe. Spika, naomba kuwasilisha.

UTARATIBU

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, kwa kuwa huu Mswada marekebisho yake tumepewa hivi asubuhi na tulikuwa tuna mambo mengi na sasa hivi zimebakia kama dakika 15 tu. Tunaomba uongozi wako utuachie haya masaa mawili tukamalizie kuyapitia haya marekebisho ili tuje tutoe mchango wenye maana hapo jioni.

Mhe. Spika: Hakuna tatizo isipokuwa wapo wajumbe ambao wapo tayari kuchangia na wameniletea maombi. Sasa nafikiri muda huu mchache tunaweza tukapata huyo mjumbe mmoja na hili wazo ambalo umelitoa litaingia bila ya kupingwa kwa pale jioni.

Basi naomba nimkaribishe Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii nikaweza kuchangia huu Mswada muhimu sana katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku hii ya leo kukutana hapa katika Baraza lako tukufu kwa madhumuni ya kufanya shughuli zetu za kawaida za Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, pili nitumie nafasi hii adhimu sana kumpongeza Mhe. Waziri wa Afya pamoja na wasaidizi wake kwa kutayarisha Mswada huu wa sheria ya kuanzisha kwa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali. Kwa kweli Mswada huu nathubutu k usema umechelewa. Kwa sababu katika kipindi chote kilichopita hakukuwa na sheria madhubuti inayosimamia chombo hiki. Hiyo ni

kasoro kubwa katika utendaji. Kwa kuwa Mhe. Waziri ameliona hili basi hatuna budi kumpongeza kwa juhudi zake alizozichukua.

Mhe. Spika, katika hotuba yangu wakati wa kupitisha sheria ya viwango Zanzibar niliishauri serikali kuanzisha sheria hii ya Mkemia. Kwa sababu sheria ile ambayo inahusiana na masuala ya viwango inauhusiano mkubwa, uhusiano wa karibu kati ya vyombo hivi viwili. Kwa sababu mfanyabiashara ikiwa hatoridhika na ripoti ambayo imetolewa na taasisi ile ya viwango basi atakata rufaa kwa Mkemia Mkuu wa serikali. Kwa wakati ule kulikuwa hakuna sheria ya kuanzishwa kwa chombo hiki. Nampongeza Mhe. Waziri kwa kuanzisha chombo hiki muhimu. Sheria hii inayoshughulikia masuala ya viwango tayari imeshasainiwa na Mhe. Rais nayo imeshaanza kazi.

Mhe. Spika, kuwa na chombo kama hichi kinachojitegemea kwa kweli ni muhimu. Lakini kiwe ni chombo kinachojitegemea kweli. Kwa maana hiyo kisiingiliwe kwa namna yoyote ile ama na mtu binafsi ama na serikali yenyewe. Tukiache kifanye kazi kwa mujibu wa sheria na wahusika waweze kufanya kazi kwa mujibu wa taaluma zao. Si vyema chombo hiki kikaingiliwa. Chombo hiki kina maamuzi ambayo yanagusa afya za watu, kinagusa haki za watu, kwa maana hiyo si vyema kikaingiliwa. Kibakie kama hivi tulivyokipitisha katika sheria au tutakavyokipitisha kwenye sheria kwamba kiwe ni chombo kinachojitegemea.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi katika Baraza hili. Katika Baraza lililopita kulikuwa kuna element za kuingiliwa ingiliwa katika vyombo vya aina kama hii. Kama tunakumbuka tulikuwa tuna suala la mchele mbovu. Mkemia aliyekuwepo wakati ule wa serikali, asubuhi alikuwa anasema mchele huu mbovu haufai kuliwa na binaadamu, lakini jioni anasema mchele huu ni safi na unafaa kuliwa na binaadamu. Kwa hivyo taarifa kama hizi kwa chombo hiki hatuzitaki tena. Tunataka taarifa zinazotolewa na chombo hiki ziwe za uhakika ambazo hazina shaka. Ndio maana nasema chombo hiki hakistahiki tena kuingiliwa na vyombo vyengine.

Mhe. Spika, kasoro moja ambayo nimeiyona katika Mswada huu ni kuhusu Mkemia kutokuwa na kinga ya kumlinda katika ufanyaji wa shughuli zake, kama vile anavyowekewa kinga Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali au Majaji wa Mahakama Kuu. Kwa sababu hawa serikali imewawekea kinga kwa makusudi kwamba akishakuteuliwa hakuna mamlaka yoyote ya kuweza kumuondosha. Hii inawapa nafasi wadhibiti na wakuguzi wakuu wa hesabu za serikali kufanya kazi zao bila ya hofu, bila ya kumuogopa mkubwa aliyekuwa juu yao au bila ya kumuogopa hata yule mtu aliyemteuwa. Kwa maana hiyo mdhibiti na mkaguzi kuu wa hesabu za serikali anafanya kazi bila ya khofu. Lakini hata majaji wa mahakama kuu na wao wanafanya kazi bila ya khofu. Rais anapomteuwa maana yake tena hana mamlaka ya kumuondosha, vyenginevyo kuwe na mambo ya msingi.

Mdhibiti na mkemia mkuu wa hesabu za serikali anayo kinga juu ya hilo, Majaji wa mahaka kuu wanayo kinga. Kwa maana hiyo hawana khofu ya kuondoshwa na wakubwa wao. Lakini Mkemia Mkuu wa Serikali yeye hana kinga. Kwa maana hiyo anaweza akapokea amri ya wakubwa waliyomzidi juu yake kwa kuhofia kuja kuondoshwa katika sehemu hii.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri katika sheria hii amuwekee kinga Mkemia Mkuu wa Serikali, pale Rais anapomteuwa maana yake tena pasiwe na chombo cha kuweza kumuondosha, *unless* kuwa na *condition* nyengine ambazo zinaweza zikamuondosha.

Mhe. Spika, tunaanzisha maabara ya Mkemia Mkuu, maabara hii inatakiwa iwe ya kisasa, kuwe na jengo lenye hadhi sio kama ilivyo sasa. Kuwe na vitendea kazi ambavyo vitamuwezesha Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya kazi zake kisasa. Kuna vyombo hapa vimetajwa kama vya *DNA* na vyengine. Hivi ni lazima vipatikane.
Mhe. Spika, Baraza lako tukufu hili limekuwa likizungumzia sana juu ya umuhimu wa chombo hiki kimekuwa hakipo Zanzibar. Tunapotaka vipimo vya *DNA* tunalazimika kupeleka *sample* zetu Tanzania Bara au Nairobi Kenya. Kwa hivyo kwa kuwa tunaanzisha taasisi hii mpya ni lazima serikali kuwa na jengo la kisasa, kuwa na vitendea kazi vya kutosha, vikiwemo vitendea kazi vya mkemia mwenyewe.

Tumeshuhudia hapa tulikuwa tunawakemia wanatembea na baiskeli barabarani. Tulikuwa tunae mkemia hapa mwenye sifa ambaye alikuwepo hapa lakini hatukumtunza na hatimaye alichukuliwa na akenda kufanya kazi Tanzania Bara. Kwa hivyo mkemia atakae teuliwa na Mhe. Rais kwanza apatiwe vitendea kazi ukiwemo usafiri, nyumba na maposho mengine. Hii itasaidia kuondosha hizi *element* za rushwa, lazima tumjenge mkemia mkuu. Kwa sababu wakati mwengine atakuwa analindwa na wafanyabiashara wakubwa wenye uwezo. Kwa hivyo ni lazima tumuwezeshe ili aweze kufanya kazi zake kwa uwadilifu, ikiwemo mishahara mizuri na maposho ambayo yanastahiki.

Mhe. Spika, kwenye vifungu vya sheria baadhi ya sheria kama kifungu cha uteuzi wa mkemia mkuu wa serikali na vifungu vyengine mimi sina mshaka navyo, vimejipanga vizuri. Isipokuwa kuna baadhi ya marekebisho ningemuomba Mhe. Waziri aangaliye kwenye kifungu cha (5) kazi za maabara. Kwa mujibu wa kifungu cha (5) (2) naomba kunukuu:-

> Kifungu cha 5(2) "Kwa mujibu wa Sharti ya kifungu cha (i) kidogo cha kifungu hiki, maabara itakuwa ni chombo cha juu na cha mwisho kuhusiana na masuala ya matokeo ya uchunguzi yanayohusiana na kazi za maabara"

Mhe. Spika, mimi kwa mawazo yangu chombo hiki tusikifunge kuwa na maamuzi ya mwisho au maamuzi ya matokeo kuwa ni cha mwisho kwa uchunguzi. Kwa sababu pengine mwananchi hakuridhika na maamuzi yaliyotolewa na Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar maana yake tumpe nafasi kukata rufaa katika vyombo vyengine ama Tanzania Bara au mahala pengine. Tunaposema kwamba kwa mujibu wa sheria Mkemia Mkuu hapa wa Zanzibar ndiye mwenye uamuzi ya mwisho, maana yake tena atakuwa hana pahala pengine kwa kwenda.

Kwa kuwa sheria zinatoa nafasi kukata rufaa kwenye Mahakama ya Rufaa ya Tanzania, basi tutoe nafasi kwa wananchi au kwa mlalamikaji kuwa na hatua nyengine zaidi ya kwenda mbele ili kuona anapata haki zake hizo. Jengine katika kifungu hiki hiki cha 5(3) naomba kunukuu.

> Kifungu cha 5(3) "Bila kuathiri masharti ya jumla ya kifungu cha (1) cha kifungu hichi kazi za maabara zitakuwa ambazo zimeainishwa (a-i)"

Mimi pendekezo langu Mhe. Spika, isiwe kufanya uchunguzi tu. Kwa sababu hapa imeelezwa kufanywa uchunguzi kuhusu masuala ya dawa na sumu. Kufanya uchunguzi wa chakula, dawa na vyenginevyo. Lakini iwe kufanya uchunguzi na kutoa matokeo. Sio kubakia kufanya uchunguzi tu bila kutoa matokeo. Kwa hivyo kila mahala ambapo panahitaji kufanywa uchunguzi katika kifungu hiki iwe kuwe na kutoa matokeo ya uchunguzi.

Mhe. Spika, chengine ni kifungu cha 21(1)(a) cha sheria hii ambacho kinazungumzia fedha kama zilivyowekwa na Baraza la Wawakilishi kama ruzuku. Hapa kidogo panakuwa na matatizo. Matatizo yanayojitokeza kwamba bajeti inayowasilishwa hapa na Mhe. Waziri anayehusika maana yake Baraza halina Mamlaka ya kuongeza hata kama tutahisi fungu hili ni dogo.

Sisi tungependa sana fungu hili liwe kubwa, liweze kutosheleza mahitaji ya chombo chenyewe na umuhimu wa chombo chenyewe, lakini Baraza halina uwezo wa kuongeza isipokuwa kupunguza fungu hilo. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri kwa kuwa sehemu hii inazungumzia masharti ya fedha. Na kwa kuwa tunazungumzia juu ya kukifanya chombo hiki kiwe bora, kiwe na vifaa vya kisasa na vyombo vya kisasa. Basi aibane serikali wakati wa kupitisha vifungu hivi kuona kwamba taasisi hii inapata fedha za kutosha. Uzoefu unaonesha kwamba mara nyingi tunaanzisha taasisi kama hizi lakini fedha ambazo tunazitoa zinakuwa kidogo mno.

Mhe. Spika, baada ya maoni hayo na muda umemalizika naomba kuunga mkono Mswada huu wa Sheria. Nimuombee Mhe. Waziri mafanikio katika kuanzisha chombo hichi, ili kiwe cha kisasa na kiwe na mtizamo wa kisasa. Ili wananchi wetu wazidi kupata matarajio ambayo wanayategemea. Mhe. Spika, naomba kuunda mkono hoja. Ahsante.

(Saa 7:00 Baraza liliakhirishwa hadi saa 11.00 jioni leo)